Nipashe
Jumamosi Oktoba 10, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580364
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**Tundu** Lissu amaliza ‘kifungo’, kuendelea kampeni Kanda ya Kati
UKURASA 2



**Mama** adaiwa kumchoma mikono mtoto kisa wizi wa Sh. 400/- za sadaka
UKURASA 3

**Pogba: Ndoto yangu ni kuichezea Madrid**
UKURASA 22

# JPM kuisuka Dar

UKURASA 2



Mgombea Urais wa CCM, Dk. John Magufuli, akiaga maelfu ya wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam, baada ya kuhutubia mkutano wa kampeni katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, jana. **PICHA: IKULU**

## Kiongozi CHADEMA auawa shambani
UKURASA 3

## Wanaume watajwa kuwa vinara magonjwa ya akili

• **Unywaji** pombe, msongo wa mawazo, vyaelezwa kuwa chanzo... *Endelea ukurasa.2*


Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store

Fursa kwa Wagombea! 2020
VOTE
Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini
Je ungependa kukishukuru chama chako ?
Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?
Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu
Nipashe MWANGA WA JAMII
Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz
VOTE

## Lissu amaliza 'kifungo', sasa kuanza Singida

**Na Romana Mallya**

MGOMBEA urais wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ametangaza leo kuendelea na kampeni zake mkoani Singida baada ya kumaliza kifungo cha siku saba cha Kamati ya Maadili ya Kitaifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi Tanzania (NEC).

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya CHADEMA, Tumaini Makene, alisema mgombea huyo alimaliza jana kifungo chake na sasa anaanza rasmi kuomba kura katika mikutano ya kampeni atakayofanya maeneo mbalimbali.

Makene alisema Lissu anatarajia leo kuendelea na kampeni zake ikiwa ni awamu ya tatu mkoani humo.

"Kesho (leo) tutaanzia Singida, ambako tutakaa huko kwa muda wa siku mbili, baada ya hapo tutakwenda Tabora na baadaye Shinyanga," alisema.

Siku saba zilizoishia jana, Kamati ya Maadili ya Kitaifa NEC, ilimsimamisha Lissu, kufanya kampeni kwa muda huo, kwa kukiuka kanuni na taratibu za uchaguzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa siku hiyo Katibu wa Kamati hiyo, Emmanuel Kawishe, iliafikiana kumsimamisha Lissu kufanya kampeni za uchaguzi kwa siku saba, kwa kukiuka maadili ya uchaguzi na kutoa lugha ya kichochezi na tuhuma zisizothibitishwa.

Taarifa hiyo ilisema Lissu ana haki ya kukata rufani kwenye Kamati ya Rufani ya NEC kupinga uamuzi huo.

Saa chache baada ya taarifa hiyo kutolewa, akizungumza na waandishi wa habari, Lissu alieleza msimamo wake kuwa ni kuendelea na kampeni.

Hata hivyo, Kamati Kuu ya CHADEMA iliyoketi kwa siku moja baada ya uamuzi wa kamati ya maadili ya Kitaifa ya NEC, iliamua kutii kusimamishwa kwa mgombea wao.

Wakati wa kifungo hicho, Lissu alitumia kofia ya Makamu Mwenyekiti na kutembelea maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam na Pwani, ambako alifungua matawi na kuonekana akinunua bidhaa.

Lissu alionekana akipanda basi la Mwendokasi kwenda Kariakoo, ambako alinunua bidhaa na kuondoka na juzi alitembelea maduka yaliyopo Mlimani City na baadaye soko la Manzese.

# Magufuli aahidi kuisuka Dar

**Na Gwamaka Alipipi**

MGOMBEA urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk.John Magufuli, amesema katika kipindi cha miaka mitano ijayo ataliisuka upya Jiji la Dar es Salaam kwa kujenga miundombinu ya kisasa na kwamba litakuwa kama Ulaya.

Watanzania na wakazi wa jiji hilo, amesema watarajie maajabu zaidi kwa kuwa kutajengwa barabara za juu (fly over) nyingi, hospitali zenye uwezo wa kutoa huduma bora, maboresho kwenye sekta ya elimu, upatikanaji wa umeme wa uhakika, pamoja na huduma bora za kijamii.

Aliyasema hayo jana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa alipohutubia maelfu ya wananchi na wanachama wa CCM waliojitokeza kumsikiliza akiomba ridhaa ya kuchaguliwa tena kuwa rais.

Dk magufuli Alisema serikali itakamilisha barabara zote ambazo hazijakamilika ikiwamo barabara ya Morocco-Mwenge, Kimara-Kibaha, Pugu- Kifuru, Mbezi Mwisho -Mpigi Magoe, Bunju- Tegeta Kibaoni, Banana -Kitunda, Kisongora- Kibamba Mloganzila.

"Nataka watu wakiteremka Dar- es- Salaam wajue wapo Ulaya na siyo Afrika. Bado nina moto wa kuijenga Dar es Salaam, mwili wangu bado una washwawashwa kuleta maendeleo katika Jiji hili. Watanzania mtegemee maajabu zaidi katika ujenzi wa miundombinu," alisema Dk. Magufuli.

Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, mradi wa mabasi yaendayo kasi awamu ya pili, tatu, nne, tano na sita utaanza kujengwa ili kurahisisha usafiri kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam.

"Wananchi wa Mbagala wataanza kufaidi mradi wa mabasi yaendayo kasi pamoja na daraja la Selandar na la Gerezani. Tutakamilisha miradi ya kimkakati ya upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa reli kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma.

"Tutapanua barabara ya bandari- uwanja wa ndege, Pugu hadi Morocco, Kawe, Ardhi-Makongo, Mbagala- Kongowe, vilevile tutaanza awamu ya tatu ya mabasi yaendayo haraka kutoka barabara ya Nyerere, Bibi Titi hadi Azikiwe," alisema.

"Awamu ya nne kutoka Maktaba, Nyerere hadi Sam Nujoma, Mwenge hadi Tegeta, awamu ya tano ya BRT ni kutoka barabara ya Mandeka, Segerea, Tabata hadi Kigogo, awamu ya sita ni kutoka Morocco, Mwai Kibaki kupitia barabara ya zamani ya Bagamoyo.

Kuhusu afya, alisema serikali inakwenda kufanya mabadiliko makubwa kwenye sekta ya afya kwa kujenga hospitali nyingi zitakazokuwa na uwezo wa kutoa huduma bora.

"Hospitali zetu za Muhimbili, MOI (Taasisi ya Tiba ya Mifupa), JKCI (Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete) tutazipelekea vifaa vya kisasa vya matibabu. Tunataka watu watoke ulaya kuja kutibiwa hapa kwetu. Tutaboresha huduma kwenye vituo vyote vya afya sambamba na kuongeza wahudumu," alisema.

Kwenye sekta ya elimu, Dk. Magufuli alisema serikali itaongeza bajeti ya fedha katika elimu ya juu, licha ya sasa kutolewa Sh. bilioni 450.

Alisema utoaji wa elimu bure kuanzia elimu ya msingi hadi sekondari utaendelea, kutajengwa maabara katika shule za sekondari, madarasa ya kutosha ili wanafunzi waweze kusoma vizuri, pamoja na kuwajengea wanafunzi uwezo wa kupata ajira.

Aidha, Dk. Magufuli aliwahakikisha wananchi wa Jiji la Dar es Salaam umeme wa uhakika, kwa maeneo yote kufikiwa na umeme ifikapo mwaka 2025.



Mgombea Urais kupitia chama cha ADC, Queen Sendiga, akihutubia mkutano wa kampeni katika Kijiji cha Ngunja, Wilaya ya Tandahimba, mkoani Mtwara jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaume waongoza magonjwa ya akili

**Na Mary Geofrey**

IDADI ya wagonjwa wa akili imeongezeka kutoka 29,166 mwaka 2018/19 hadi 33,287 mwaka 2019/20 huku wanaume wakiongoza, imeelezwa.

Haya yalisemwa jana ikiwa leo ni Siku ya Afya ya Akili Duniani na kwamba idadi hiyo ya wagonjwa ni wale kwa waliotibiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Upanga na Mloganzila, jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, kati ya wagonjwa hao idadi ya wanaume ni kubwa ambao walikuwa 18,535 kulinganisha na wanawake ambao walikuwa 10,631 kwa mwaka 2018/19.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Afya ya Akili MNH, Dk Fileuka Ngakongwa, aliyabainisha hayo jana mbele ya waandishi wa habari wakati akizungumzia maadhimisho hayo.

Akizungumzia sababu za wanaume wengi kuugua matatizo ya akili na kupata ugonjwa huo katika umri mdogo, ukilinganisha na wanawake, alisema ni kutokana na msongo wa mawazo, ugumu wa maisha na kuweka vitu moyoni kulinganisha na wanawake ambao huzungumza.

"Uwiano wa ugonjwa huu wa akili kati ya wanaume na wanawake ni mbili kwa moja, wanaume ni wengi ukilinganisha na wanawake," alisisitiza.

Alieleza sababu nyingine za ugonjwa huo ni uwezo binafsi wa kuchanganua changamoto anazopitia kwenye maisha na jamii inayomzunguka.

Alisema pia mazingira ya watu wanayoishi, wanayofanyia kazi, kukosa amani, vinasaba vya akili na magonjwa ya mwili kama Malaria, Homa ya Kichwa na Uti wa Mgongo, ajali ya kichwa na wenye maambuzi ya UKIMWI kwenda kichwani na magonjwa yasiyoambukiza.

"Niwasihi Watanzania kujitokeza kupata huduma za afya pindi wanapohisi kuwa na dalili za ugonjwa huu wa akili kwa sababu unatibika kwa muda mfupi endapo mgonjwa atawahi hospitali," alisema Dk. Ngakongwa.

Alitaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni kukosa usingizi, unywaji wa pombe kupita kiasi, woga uliopitiliza, mtoto kukojoa kitandani katika umri ambao alishapita hatua hiyo.

Alisema licha ya kutoa huduma hiyo kwa mafanikio makubwa kuna changamoto ya wagonjwa kutelekezwa hospitali kuwaleta ndugu huku wakiacha ... 

Dk. Ngakongwa alisema, ndugu wa wagonjwa wanapofika hospitali kuwaleta ndugu huwaacha solemba hivyo, hospitali hulazimika kuwatafuta ndugu zao mahali popote nchini na kutoa matangazo kwenye vyombo vya habari kwa sababu matibabu yake huusisha familia na watoa huduma.

# Mama adaiwa kumchoma mtoto mikono kisa wizi 400/- sadaka

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

JESHI la polisi mkoani Rukwa linamshikilia Stella Kangoza (29) mkazi wa Kitongoji cha Kaloleni kata ya Lwiche, Manispaa ya Sumbawanga kwa tuhuma za kumfanyia ukatili mtoto wake.

Mwanamke huyo anadaiwa kumchoma moto mikono kwa madai kuwa ameiba Sh. 400 mtoto huyo mwenye umri wa miaka tisa (jina linahifadhiwa), ambaye ni mwanafunzi wa darasa la tatu (jina la shule linahifadhiwa) .

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Justin Masejo, alisema jana kuwa tukio hilo lililotokea Oktoba 4, mwaka huu, majira ya saa 2:00 usiku mara baada mama huyo kurudi nyumbani na kuitafuta pesa hiyo, bila mafanikio.

Alisema baada ya mama huyo kutoka katika shughuli zake, alianza kuitafuta pesa hiyo aliyokuwa ameikweka ndani kwa lengo la kutoa sadaka kanisani, lakini hakuipata.

Baada ya kuitafuta kwa muda mrefu bila mafanikio, alisema ndipo alipomwita mtoto wake na kumuuliza na kukiri kuichukua na kwenda kununua maandazi baada ya kusikia njaa, ambayo ilimuuma kwa muda mrefu kwa kuwa mama yake aliondoka nyumbani, bila kumwachia chakula.

Mtoto huyo alipomjibu mama yake, alisema ndipo alipokasirika na kuanza kumpiga na kuamua kumchoma mikono yake, kwa madai kuwa tukio hilo halikuwa la kwanza kwa mtoto huyo kwa sababu alikuwa akimfumbia macho na bila kufanya hivyo atakuwa mwizi.

Kutokana na kitendo hicho, uongozi wa serikali ya mtaa ulipata taarifa za tukio hilo na kwenda kutoa taarifa katika kituo cha polisi na hatimaye mwanamke huyo kukamatwa.

Kamanda Masejo alisema mwanamama huyo anashikiliwa na polisi kwa mahojiano na kwamba atapelekwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Alitoa onyo kwa wazazi mkoani hapa kuacha kuwaadhibu watoto wao pindi wanapokuwa na hasira kwa kuwa matokeo yake yamekuwa mabaya na kuwaacha watoto wao na ulemavu wa kudumu.

## Kiongozi wa CHADEMA auawa akiwa shambani

**Na Elisante John,** SINGIDA

KATIBU Mwenezi wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kata ta Mhintiri, Ikungi mkoani Singida, Nicholaus Andrea, ameuawa na watu wasiojulikana akiwa shambani kwake.

Kiongozi huyo ambaye pia ni meneja kampeni wa mgombea udiwani wa kata ya Mhintiri, Christina Ntembo, aliuawa juzi akiwa anaandaa shamba kwa ajili ya msimu ujao.

Kutokana na mauaji hayo, Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Ikungi, Omari Toto, amelitaka jeshi la polisi kufanya uchunguzi kutokana na utata uliotawala juu ya kifo hicho.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Singida, Sweetbert Njewike, alisema jana kuwa, mwili wa marehemu ulikutwa ukiwa na majeraha sehemu mbalimbali za mwili, yaliyotokana na kukatwa na kitu chenye ncha kali.

Njewike alibainisha kuwa uchunguzi wa awali unaonyesha mauaji hayo yametokana na wivu wa mapenzi na tayari Samweli Alute, aliyekuwa mume wa Pendo Omari, aliyekuwa na uhusiano wa kimapenzi na Andrea, anashikiliwa na polisi kwa ajili ya uchunguzi zaidi,

Uongozi wa CHADEMA Wilaya ya Ikungi ulisema Andrea alitarajiwa kuzikwa jana kijijini kwao, Muhintiri, huku mazishi yake yakitarajiwa kuongozwa na viongozi mbalimbali wa chama hicho, wakiwamo wa Kanda ya Kati, chini ya Mwenyekiti wake, Lazaro Nyalandu.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, akionyesha moja ya vielelezo kwa waandishi wa habari, jijini Mwanza jana, baada ya kuwakamata watu 12 kwa tuhuma za kujihusisha na makosa mbalimbali ya kiuhalifu ikiwamo utapeli na kuchana mabango ya wagombea wa vyama vya CCM na CHADEMA. **PICHA: NEEMA EMANNUEL**

# Wakamatwa kwa madai ya utapeli, kuchana mabango

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mwanza, linawashikilia watu 12 kwa tuhuma za kujihusisha na matukio ya uhalifu ikiwamo la utapeli na kuchana mabango ya wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Jumanne Muliro, alisema jana kuwa katika matukio hayo, watu wanne wamekamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na utapeli.

Muliro alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa na Dola za Kimarekani 192 katika mchanganuo wa noti moja ya Dola 100 na noti 92 za Dola moja moja, ambazo ni sawa na Sh. 441,000 za Kitanzania .

Pia alisema watu hao walikamatwa wakiwa na Sh. 127,000 za Kitanzania na makaratasi yaliyokatwa mithili ya noti yaliyofungwa kwa pamoja na kuwekwa kwenye bahasha.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Yelemi Athuman (45) mkazi wa Dar es Salam, Mussa Juma (44) mkazi wa Muleba, Rutayisire Mande (38) raia wa Uganda na Delphina Kungu (51) mkazi wa Singida.

Watuhumiwa hao, alisema kwa pamoja walikamatwa na gari namba T.205 BGW aina ya Toyota Chaser rangi nyeupe ambalo alisema wanalitumia katika kutenda uhalifu katika maeneo mbalimbali.

"Baada ya kuwahoji kwa kina watuhumiwa hao wamekiri kujihusisha na matukio ya utapeli katika mikoa mbalimbali ya nchini yakiwamo Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Tanga, Kigoma na baadhi ya nchi jirani zikiwamo Uganda, Zambia na Kenya," alisema.

Akieleza watuhumiwa hao wa utapeli wanavyofanya kazi, Muliro alisema walieleza mbinu wanazotumia kuwa ni kwenda ndani ya benki na kujifanya hawana uelewa wa taratibu za kubadilisha fedha za kigeni kwa kutaja kiwango cha chini cha ubadilishaji wa Dola na kuomba msaada kwa mteja waliyemlenga.

Baada ya kubaini kuwa ana fedha nyingi, ili awasaidie kujaziwa fomu na baadaye mteja huyo akikubali na kuingia tamaa ya kupata faida kirahisi, wanamrubuni na kutoka naye nje ya benki.

Alisema baada ya kutoka naye kwenda sehemu nyingine, mara nyingi hutumia maeneo ya hoteli ambako ndiko utapeli huo hufanyika kwa kujipatia fedha halali za Kitanzania zenye thamani kubwa na wao kumpatia anayetapeliwa bahasha yenye makaratasi na wakati mwingine dola yenye thamani ndogo.

Katika tukio lingine, Muliro alisema watu wanane wamekamatwa kwa tuhuma za kuchana mabango ya wagombea wa ubunge na udiwani kutoka CHADEMA na CCM katika maeneo tofauti ya Wilaya ya Nyamagana.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Masalu Bululi (24), Steven Augustino (22), John Juma (20), Amani Stephano (33) na Abuu Abubakary (28) ambao wameshafikishwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha miezi mitatu kila mmoja.

Pia aliwataja watuhumiwa wawili, ambao kesi ziko mahakamani ni Samwel Matongo (32) na Seleman Issa (25 ) huku mtuhumiwa Abbas Gerald (33) upelelezi ukiwa bado unaendelea.



Mgombea Mwenza wa Kiti cha Urais kwa tiketi ya CCM, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na kuzungumza na wanachama wa chama hicho, na wananchi wa Kijiji cha Magula Sitalike, mkoani Katavi, akiwa njiani kuelekea mkoani Rukwa, kwa ajili ya kuanza ziara ya kampeni za uchaguzi. **PICHA: OMR**

## IGP Sirro aonya vurugu uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, amesema hali ya kisiasa nchini imeendelea kuimarika hasa wakati huu wa kampeni za uchaguzi mkuu na wananchi wengi wamekuwa watulivu.

Hata hivyo, amesema wako baadhi ya watu wachache walioandaliwa na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa kufanya vurugu na kujiingiza kwenye uhalifu.

IGP Sirro aliyasema hayo jana, jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari na kuwataka baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa kufanya masuala ya siasa na kuacha kuwatumia vijana katika uhalifu.

Kutokana na viashiria hivyo, alisema yeyote atakayebainika atachukuliwa hatua za kisheria huku akiwataka wananchi kuepuka vishawishi vya kujiingiza kwenye uhalifu.

Alisema watu hao wanabeba matatizo ya wengine kwa kupata shida kutoka kwa baadhi ya wanasiasa wasiowatakia mema na kushindwa kutimiza ndoto zao.

Kuhusu upigaji wa kura Zanzibar, IGP Sirro alisema kuna baadhi ya watu wanaohamasisha watu au kikundi cha watu kuvunja sheria wakati wa upigaji kura kinyume cha sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Pamoja na kuwapo kwa taarifa hizo, alisema upigaji kura utafanyika kwa mujibu wa tarehe iliyopangwa na utafanyika kwa amani na utulivu na kuwapata viongo-

## ‘Nyumba ni Choo’ yapunguza magonjwa ya kuambukiza

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPENI ya Taifa ya Usafi wa Mazingira, ‘Usichukulie Poa Nyumba ni Choo’ na mradi wa Huduma Endelevu za Maji na Usafi wa Mazingira, imefanikiwa kupunguza magonjwa ya kuambukiza ikiwamo kipindupindu.

Imeelezwa kuwa kwa sasa kaya nyingi zimeelimika kwa kunawa mikono na zisizokuwa na vyoo zimepungua kutoka asilimia 6.1 mwaka 2015/16 hadi asilimia mbili mwaka 2019/20.

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, aliyasema hayo jana wakati akitoa tamko la serikali kuhusu siku ya Afya Mazingira Duniani.

Dk. Subi alisema zaidi ya Sh. bilioni 40.2 zimepelekwa kwenye mikoa na Halmashauri kwa ajili ya usafi wa mazingira.

“Fedha hizi ni nyingi na haya ndiyo matunda ya uwekezaji kwenye masuala ya afya kwa wananchi moja kwa moja, kila mwananchi mtoto wake anakwenda shule anahitaji anywe maji, kampeni hizi zinaleta mafanikio makubwa katika jamii,” alisema.

Alisema mwaka 2015 ugonjwa wa kipindupindu ulikuwapo lakini umepotea tangu Julai, mwaka jana.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Afya Mazingira kutoka wizarani hapo, Anyitike Mwakitalima, alisema maeneo ya mijini ipo ahueni kubwa ya upatikanaji wa maji kwa asilimia 86 na vijijini asilimia 70.

Naye Ofisa wa Afya Mazingira, Yusuph Seif, aliwataka wamiliki wa mabasi kuyasimamisha magari yao kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya huduma za vyoo bora, sehemu za kunawia mikono kwa maji tiririka na sabuni.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Muslim alisema watu kwenda porini kujisaidia siyo ustaarabu.

“Katika mabaraza yetu, askari wetu tuwaambie watoe elimu ili madereva wawapeleke watu sehemu zenye huduma ya kijamii,” alisema.

## Waombaji 60,600 wadahiliwa vyuo vikuu

**Na Romana Mallya**

WAOMBAJI 60,621 kati ya 90,572 walioomba nafasi katika taasisi za elimu ya juu awamu ya kwanza ya udahili kwa ngazi ya shahada ya kwanza, wamepata nafasi.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Prof. Charles Kihampa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akitangaza kukamilika kwa awamu ya kwanza na kufunguliwa kwa awamu ya pili ya udahili.

Alisema waliodahiliwa kwa awamu ya kwanza ya mwaka wa masomo 2020/21 ni sawa na asilimia 69.9.

Prof. Kihampa alisema kwa mwaka wa masomo 2019/20, waombaji walikuwa 83,197 na waliodahiliwa walikuwa ni 51,385 wakati mwaka 2018/19 waombaji walikuwa 74,113 na waliodahiliwa walikuwa ni 43,005.

Alisema waombaji wa udahili kwa mwaka wa masomo 2020/21 walituma maombi ya kujiunga katika vyuo 74 vilivyoidhinishwa kudahili katika awamu hiyo ya kwanza.

“Jumla ya programu 686 zimeruhusiwa kudahili ikilinganishwa na programu 645 mwaka 2019/20. Kwa upande wa nafasi mwaka huu kuna nafasi 157,770 ikilinganishwa na nafasi 149,809 mwaka uliopita,” alisema.

Prof. Kihampa alisema hilo ni ongezeko la nafasi 7,961 za shahada ya kwanza sawa na asilimia 5.3.

“Mwenendo wa udahili kwa kipindi cha miaka mitatu kati ya mwaka wa masomo 2018/19 hadi 2020/21 unaonyesha ongezeko kubwa la waombaji ikiashiria ongezeko la wahitimu wa Kidato cha Sita na wa Stashahada,” alisema.

“Wasiodahiliwa mwaka 2018/19 walikuwa 31,108, mwaka 2019/20 waliongezeka na kufikia 31, 812 na mwaka huu wa masomo 2020/21 ni 32,120. Waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja mwaka 2018/19 ni 16,507, mwaka 2019/20 walikuwa 20,858 na mwaka huu 2020/21 wamefikia 28,501,” aliongeza.

Prof. Kihampa aliwataka waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja, wahakikishe wanathibitisha udahili wao katika chuo kimojawapo kuanzia jana hadi Jumapili ijayo, kwa kutumia ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri watakaotumiwa kwenye simu au barua pepe.

“Wale ambao hawatapata ujumbe huu kwa wakati, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri, ili wajithibitishe,” alisema.

Kuhusu awamu ya pili ya udahili, Prof. Kihampa alisema dirisha lake linafunguliwa kwa muda wa siku sita kuanzia Jumatatu ijayo, hadi Oktoba 18.

Alisema waombaji ambao hawakuweza kutuma maombi ya udahili au hawakudahiliwa katika awamu ya kwanza kutokana na sababu mbalimbali, watumie fursa hiyo.

“Tunawahimiza waombaji na vyuo kuzingatia utaratibu wa udahili kwa awamu ya pili kama ilivyoonyesha kwenye kalenda ya udahili iliyotolewa na TCU iliyoko kwenye tovuti,” alisema.

Pia alitoa wito kwa waombaji wa shahada ya kwanza kuwa masuala yote yanayohusu udahili na kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika.

Prof. Kihampa alivitaka vyuo kujipanga kupokea wanafunzi zaidi hapo baadaye kwa sababu elimu bure itatoa vijana wengi wenye sifa za kujiunga na vyuo vikuu.

HABARI KITAIFA

# TAKUKURU ilivyookoa mil. 191/- miezi mitatu

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Geita, imeokoa kiasi cha Sh. 191,198,624.92 zilizokuwa zimefanyiwa ubadhirifu kwa njia za rushwa, dhuluma na ukopeshaji unaoumiza.

Kamanda wa TAKUKURU Mkoa wa Geita, Leonidas Felix, akitoa taarifa ya utekelezaji wa taasisi hiyo kwa wanahabari wa mkoa huo, alisema fedha hizo zimerejeshwa baada ya ufuatiliaji uliofanywa na taasisi hiyo kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu.

Kamanda huyo alisema fedha hizo zimerejeshwa serikalini, vyama vya ushirika vya kuwekana kukopa (SACCOS) zikiwamo Sh.milioni 5.5, ambazo mwalimu mstaafu, Adela Andrea Faustine. Mkazi wa wilayani Chato aliyekuwa amedhulumiwa na mkopeshaji, Isack Maswi wa wilayani Chato.

Kamanda huyo akimkabidhi fedha mwalimu huyo mstaafu, alisema taasisi hiyo inaendelea kumchunguza mkopeshaji huyo, aliyekuwa amemkopesha mwalimu huyo Sh. 700,000, na baada ya mwalimu huyo kulipwa fedha yake ya kustaafu, inadaiwa alipewa vitisho na mkopeshaji huyo, hivyo kulipa kiasi cha Sh. 7,000,000 ambayo ni sawa na asilimia 900 .

Alisema TAKUKURU ilimkuta mkopeshaji huyo pia akiwa na kadi za benki 64 za wakopaji wengi wakiwa ni watumishi wa umma. Leonidas alisema Sh. 30,124,323.zimeokolewa na kurejeshwa kwenye SACCOS pamoja na chama cha wachimbaji wadogo (Geita SACCOS) ambayo imerejeshewa Sh. 13,194,323. Chama cha wachimbaji wadogo cha Ikuzi wilayani Bukombe Sh. 16,630,000 na Katoma SACCOS ya wilayani Geita Sh.300,000.

Alisema fedha nyingine zilizookolewa na kurejeshwa serikali ni Sh. 47,967,301.2 kutoka ushirika wa Nyamatagata ambazo zilitakiwa kulipwa kodi serikalini katika biashara wanayofanya ya kuuza vyuma chakavu kutoka mgodi wa Dhahabu Geita Gold (GGML) .

"Nilikaa kwa miaka miwili nikiwa natafuta risiti niliyotumia kumlipa huyo mkopeshaji ... baada ya kuipata niliamua kwenda ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Chato, hivyo nawapongeza maofisa hao pamoja na kamanda wa Mkoa kwa msaada wao, wametenda haki," .alisema mwalimu Adela.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa fedha hiyo, alisema makubaliano ya mkopo huo ilikuwa ni kurejesha riba ya asilimia 50 kwa laki moja kwa muda wa miezi sita, lakini baadae mkopeshaji huyo alimpa vitisho na kumtaka Sh.milioni saba.




Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Benjamin Mkapa, Itale John (kushoto), akitoa mada kwenye maadhimisho siku ya mtoto wa kike duniani, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa C-Sema, Kiiya JK (kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Welfare Consultant, Veronica John (wa pili kulia) na Meneja Miradi Global Peace Fourdation Tanzania, Irene Ishengoma. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tanzania, China kuimarisha uhusiano kimkakati

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA na China zimekubaliana kuendeleza uhusiano ya kimkakati ili kuwezesha uwapo wa ulingo sawa miongoni mwa mataifa katika kusimamia maslahi na maendeleo ya nchi husika katika jumuiya za kimataifa.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliyasema hayo jana Dar es Salaam alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa China nchini, Wang Ke.

Katika mazungumzo hayo, Prof. Kabudi alisisitiza umuhimu wa mataifa kuheshimiana na kutokubali kuingilia uhuru wa mambo ya ndani ya nchi kwa kisingizio cha haki za binadamu, demokrasia au jambo lolote lingine.

Aliongeza kuwa mazungumzo hayo ya kimkakati yalilenga pia kutambua kuwa mwaka huu ni mwaka wa 55 tangu Tanzania na China zitie saini mkataba wa urafiki ambao uliweka msingi wa uhusiano makubwa na ya dhati katika nyanja mbalimbali.

Prof. Kabudi alizitaja Nyanja hizo kuwa ni ulinzi na usalama, afya, kilimo, elimu na miundombinu huku akibainisha kwamba mpaka sasa China ni taifa linaloongoza nchini kwa uwekezaji wa moja kwa moja.

Kwa mujibu wa Waziri Kabudi, China imewekeza zaidi ya miradi 700 yenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 7.1 na kutengeneza zaidi ya ajira 87,000 kwa Watanzania.

Kwa upande wake, Balozi Wang alisema China wakati wote ni rafiki mwaminifu na wa kudumu wa nyakati zote kwa Tanzania na kwamba kutimiza miaka 55 ya urafiki wa nchi hizo ni kielelezo tosha na siku zote wataendelea kuuheshimu na kuuenzi urafiki huo.

Katika hatua nyingine, Prof. Kabudi alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Finland nchini, Riitta Swan pamoja na Balozi wa Canada nchini, Pamela O'Donnell.

Prof. Kabudi na mabalozi hao, pamoja na mambo mengine, walijadili masuala mbalimbali ikiwamo kuimarisha mahusiano, uwekezaji na biashara, afya, elimu pamoja na utalii.

# Majaliwa asema uongozi si mzaha

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amesema wananchi wanatakiwa watafakari kwa kina wakati wanapochagua kiongozi.

Amesema uongozi wa nchi si jambo la mzaha wala la majaribio, hivyo ni lazima apatikane mtu makini atakayeleta maendeleo.

Majaliwa aliyasema hayo jana alipozungumza na wananchi wa jimbo la Mlalo wilayani Lushoto, Tanga katika mkutano ya kumwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Rais John Magufuli, mgombea ubunge jimbo la Mlalo, Rashid Shangazi na wagombea udiwani kwa tiketi ya CCM.

"Lazima tujue historia yake kiutumishi tusimchague mtu kwa kuwa amepanda kwenye jukwaa kwa mbwembwe, lazima tupate kiongozi atakayeweza kutuunganisha Watanzania wote na atakayetunza amani. Lazima tupate kiongozi atakayewasaidia wanyonge naye ni Dk. John Magufuli, mgombea urais kwa tiketi ya CCM," alisema.

Majaliwa alitumia fursa hiyo kuwaomba Watanzania wote wawachague wagombea wa CCM katika ngazi ya urais, ubunge na udiwani kwa sababu wanatoka katika taasisi yenye uwezo wa kuwatumikia wananchi wote bila ya kujali itikadi za aina yoyote.

Alisema wananchi wanatakiwa kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura, Oktoba 28, mwaka huu, na kumchagua Dk. Magufuli katika nafasi ya urais kwa sababu tayari wameshuhudia kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

"Tukamchague Dk. Magufuli aendelee kusambaza maendeleo," alisema Majaliwa.

Alisema maendeleo hayana chama hivyo wananchi wote bila ya kujali itikadi za vyama vyao wahamasishane kwenda kumchagua Dk. Magufuli ambaye ni kiongozi atakayeshirikiana nao katika kutatua changamoto zinazowakabili katika maeneo yao kwa kutumia Ilani ya uchaguzi ya CCM, ambayo imeainisha kila kitu.

Alisema Rais Magufuli anataka kuona kila nyumba ya Mtanzania inapata umeme tena kwa gharama nafuu na ametenga fedha nyingi zitakazotosheleza kusambaza umeme katika vijiji vyote vikiwamo na Wilaya ya Lushoto.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mashabiki wanakumbushwa kuishangilia Stars nyumbani

**TIMU** ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kucheza mechi yake ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya majirani zao, Burundi, kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Mechi hiyo inatambuliwa katika Kalenda ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), hivyo matokeo yake yatasaidia kuipandisha au kuishusha Tanzania kwenye orodha ya viwango duniani.

Si tu mchezo wa kirafiki, lakini ni sehemu ya maandalizi kuelekea mchezo wa kwanza wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika dhidi ya Tunisia utakaochezwa jijini Tunis, ifikapo Novemba 13, mwaka huu.

Marudiano ya mchezo huo unaosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), utachezwa Novemba 17, mwaka huu hapa nyumbani.

Katika mashindano hayo, Tanzania maarufu Taifa Stars imepangwa Kundi J, ikiwa pamoja na Equatorial Guinea na Libya.

Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, anatarajia kutumia mchezo wa kesho kuwaweka fiti wachezaji wake kwa ajili ya kuwakabili Waarabu hao wa Tunisia, lakini akihitaji kuibuka na ushindi.

Tunafahamu shabiki ni mchezaji wa 12 uwanjani, hivyo ni jukumu letu wananchi wa Dar es Salaam na mikoa jirani kujitokeza kwenda kuwashangilia wachezaji wetu ili watupe matokeo ya furaha katika mchezo huo utakaoanza saa 10:00 jioni.

Kama mdau wa soka unahitaji wachezaji wapambane kusaka matokeo chanya katika mechi hiyo ya kesho na nyingine za hatua ya makundi zitakazofuata, ni wakati sahihi wa kujitambua pia kama shabiki kutimiza majukumu ya kwenda kuwashangilia.

Mchezaji anapocheza kwenye uwanja wa nyumbani uliojaa, humwongezea hamasa ya kupambana na kujiona ana deni la kuwafurahisha Watanzania wenzake, na ili kutimiza hili, ni vyema mashabiki wakafika uwanjani kwa wingi kuwashangilia 'askari' wao.

Kufanya vyema kwa Taifa Stars kutasaidia kuwavutia mawakala kuifuatilia timu hii na hatimaye kuwatafutia wachezaji wetu klabu za Ulaya kama ambavyo nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta anavyoitangaza Tanzania kimataifa.

Hakuna kisichowezekana, twendeni tuaishangilia Stars ili siku za usoni Tanzania iwe na nyota wengi wanaocheza soka la kulipwa kama walivyo Burundi na Uganda kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, wamekuwa na idadi kubwa ya wachezaji wa kulipwa ukilinganisha na nchi nyingine za ukanda huu.

Kama ambavyo mashabiki hujitokeza kuzingalia timu zao pendwa za Simba na Yanga zinapokutana, huu ni wakati wa kuonyesha mahaba kama hayo kwa nchi na kwa kufanya hivyo, itasaidia 'kuwatisha' wapinzani ambao watakuwa wamekuja kwa kazi moja tu ya kusaka ushindi.


Huu ni wakati wa mashabiki kuungana na kuweka tofauti pembeni, huku mkitakiwa kushangilia kwa nidhamu na kujiepusha na vitendo ambavyo vinaweza kuigharimu nchi kutokana na kila tukio katika mechi hizi zinazokuja kurekodiwa na kupelekwa CAF, kama jambo baya litakuwa limefanyika.

Stars ikipata mashabiki wengi, hiyo itakuwa ni mafanikio makubwa tayari itajiweka kwenye mazingira ya ushindi kwa kuwaogopesha wapinzani.

Inafahamika Waarabu wamekuwa na matukio ya 'fitna' timu zetu zinapokwenda kwao, lakini Watanzania tusijikite kwenye mbinu chafu na badala yake kuwekeza katika maandalizi sahihi pamoja na kushangilia kwa ustaarabu.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Taifa Stars.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Upendeleo hauleti ufanisi

Na Barnabas Maro

**'UPENDELEO'** ni hali, tabia au tendo la kupendelea. Tabia ya kufanya jambo kwa kumili, yaani kitendo cha kitu au mtu kuelemea upande mmoja kimawazo au kimatendo.

Ndivyo inavyoonekana kuwa hivyo kwa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kuzipendelea Simba na Yanga kwenye mechi za Ligi Kuu kwa kisingizio kisichokuwa na mantiki, yaani mpangilio wa mawazo unaoweza kutumika kuunda hoja inayofaa; taaluma inayohusu kanuni za kufikiri kwa hoja.

Timu zinazoshiriki Ligi Kuu nchini zaruhusiwa kusajili wachezaji 30 kila moja. Wanaosajiliwa ni wachezaji wa kigeni na Watanzania. Maana yake kila mchezaji anayesajiliwa amethibitishwa kwa ubora. Siamini kuwa hata wakipungua wachezaji wanne au sita timu itakosa wachezaji muhimu. Kama ndivyo, maana ya kusajili wachezaji 30 ni nini na kama waliobaki baada ya kutokuwapo wachezaji wanne au watano hawafai, kwa nini walisajiliwa?

Pia ikumbukwe mchezaji asipochezeshwa ingawa hufanya mazoezi na wenzake, ndivyo uwezo na ubora wake unavyopungua na kujilaumu kimoyo moyo ni kwa nini alikubali kusajiliwa na timu husika ilhali hapewi nafasi ya kucheza.

Simba na Yanga zilikuwa zipambane Oktoba 18, mwaka huu, lakini Bodi ya Ligi (TPLB) ikapeleka mbele mpaka Novemba 7, mwaka huu licha ya Taifa Stars kuwa na mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) dhidi ya Tunisia ambazo zote zipo Kundi 'J' pamoja na Libya na Equatorial Guinea.

Stars itaanza kwa kuwafuata Tunisia mchezo utakaochezwa Novemba 13 na marudiano yakiwa ni Novemba 17, mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

Ni ukweli usiopingika kuwa timu za Simba na Yanga ndizo zinazoipa TFF na timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu fedha nyingi zaidi ya timu zingine. Simba au Yanga zinapocheza Dar es Salaam au nje, wanaojaza viwanja ni wanachama, wapenzi na mashabiki wa timu hizo walioenea nchi nzima.

"Fedha ilivunja nguu, milima ikalala." Maana yake pesa zina uwezo wa kuivunja milima na vilima. Methali hii hutumiwa kupigia mfano uwezo wa fedha. Mtu akiwa na pesa anaweza kufanikiwa kufanya mambo ambayo asingeweza kuyafanya wala kudhania kuyafanya.

Wakati Simba wakiridhia mabadiliko hayo, ilhali wachezaji wao, Luis Miquissone wa Msumbiji, Meddie Kagere wa Rwanda na Joash Onyango wa Kenya wameitwa kwenye timu zao za nyumbani, hakuna wachezaji wa kigeni wa Yanga walioitwa makwao. Msemaji wa Yanga, Hassan Bumbuli amesema viongozi wao wamepokea kwa mikono miwili uamuzi huo kwa kuheshimu mamlaka na kuweka wazi kuwa wamejipanga kwa mechi zingine kabla ya kupambana na watani wao (Simba). Kwamba moto wao ni ule ule kama ilivyokuwa msimu uliopita! Je, maneno aliyosema Bumbuli yana mantiki? Angesema hivyo kama baadhi ya wachezaji wao wanaotegemewa wangeitwa makwao?

Tena anasema: "Moto wetu ni ule ule kama wa msimu uliopita." Twajua msimu uliopita Simba ilitwaa mataji matatu: Ngao ya Hisani, Kombe la FA na Kombe la Ligi Kuu. Je, Yanga ilitwaa nini msimu uliopita hata msemaji wake aseme: "Moto ni ule ule kama msimu uliopita?" Kauli hiyo ilistahiki kutolewa na Msemaji wa Simba inayosubiri kupambana na mabingwa wa nchi zingine lakini si Yanga isiyokuwa na chochote chochote cha kujivunia msimu uliopita!

"Maneno ni kama fumo, yakitoka mdomoni hayarudi." Maana yake neno analotamka mtu ni kama mkuki (fumo), likitoka halirudi na huweza kuleta madhara. Twanasihiwa tuwe na tabia ya kuyatafakari maneno tuyasemayo kabla ya kuyasema. Ni vizuri kulipima neno kabla ya kulisema na kujiletea majuto baadaye. Je, 'moto ni ule ule' wa kujikongoja (kwenda kidogo kidogo kwa takilifu kutokana na uzee au ugonjwa) bila kutwaa chochote? Msemaji wa Yanga apaswa kusema: "Lahaula!" yaani tamko linalotumiwa na mtu anapotanabahi baada ya kusahau au kushtukia jambo.

Kero nyingine ni baadhi ya waamuzi kutofuata kanuni na sheria za mchezo wa kandanda. Watazamaji huona mengi yafanywayo na waamuzi wa kati au wasaidizi wao na kusababisha malalamiko ya timu zinazonyimwa penalti za wazi ilhali hata mchezo unaporudiwa tena na tena kwenye runinga unaona dhahiri kuna upande umeonewa kwa njia moja au nyingine.

Aidha, mara nyingi mipira inayotoka nje ya uwanja, warushaji hutakiwa kurusha mipira sehemu ile ile iliyotokea lakini warushaji huenda hatua nne mpaka tano kutoka eneo ulipotokea mpira bila kutakiwa kurusha mpira eneo ulipotokea!

Kuna makosa yanayotokea uwanjani lakini ama hayaonekani na wasimamizi au hata kama yakionwa hufumbiwa macho! TFF yapaswa kuwa makini na makosa kama hayo.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# RC Moro ataka wenye viwanda kushiriki maonyesho ya bidhaa

**Na Mwandishi Wetu, MOROGORO**

MKUU wa Mkoa wa Morogogo, Loata Ole Sanare, amewataka wamiliki wa viwanda mkoani hapa, kushiriki Maonyesho ya Tano ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania ili kupanua ujuzi.

Amesema hatua hiyo itawawezesha kuviendesha viwanda na kutumia fursa ya kukutana na wamiliki na wenye viwanda kutoka mikoa mingine na kubadilishana uzoefu.

Sanare aliyasema hayo jana kwenye kikao cha kujadili ustawi wa maendeleo ya viwanda kwa Mkoa wa Morogoro kilichowakutanisha wamiliki wa viwanda wa mkoa huo na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade). Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na TanTrade, Sanare alisema uwekezaji kwenye viwanda umepewa kipaumbele na serikali ambapo utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (1996 - 2020) yenye malengo ya kuiwezesha sekta ya viwanda kuchangia kufikia malengo ya maendeleo ya muda mrefu kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Alihimiza wawekezaji kuanzisha viwanda hususan vidogo vidogo vya kusindika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kupanua wigo wa ajira kwa wananchi na kuwataka wakuu wa wilaya kuhakikisha wawekezaji kwenye maeneo yao wanajadili kila mara changamoto wanazokutana nazo ili kuboresha uwekezaji nchini

Nae Mkurugenzi wa Ukuzaji wa Biashara kutoka TanTrade, Boniface Michael, aliwaomba wamiliki wa viwanda kwa Mkoa wa Morogoro kutumia jukwaa hilo la maonyesho ya bidhaa za viwanda yanayoandaliwa na TanTrade ili kupanua wigo wa masoko nje ya mkoa kwa lengo la kuimarisha soko la ndani.

Kwa kufanya hivyo, pia alisema watatambulisha bidhaa wanazozalisha kwa Watanzania ili kuchochea uzalishaji, kuwaunganisha wenye viwanda na wazalishaji mbalimbali wa malighafi na huduma zingine zinazotumika viwandani na kuwaunganisha wenye viwanda na wasambazaji wa teknolojia ya viwanda.

Maonyesho hayo yamebeba kaulimbiu ya "Tumia Bidhaa za Tanzania, Jenga Tanzania" ili kuhamasisha Watanzania waendelee kupenda, kununua na kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda nchini. Maonyesho hayo yanatarajiwa kufanyika Desemba 3 hadi 9, mwaka huu, katika uwanja wa Maonyesho wa Mwl J.K.Nyerere Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.



Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Simon Karikari, akijibu maswali na kutatua matatizo ya wateja wa Tigo katika kituo cha huduma kwa wateja, kama sehemu ya wiki ya huduma kwa wateja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ulongoni kicheko kujengewa daraja

**Na Mary Geofrey**

WANANCHI wa mtaa wa Ulongoni, kata ya Gongo la Mboto, Ilala jijini Dar es Salaam, wanatarajia kuondokana na adha ya kukatika kwa mawasiliano, baada ya mradi wa ujenzi wa daraja la Ulongoni A kutarajiwa kukamilika Aprili, mwakani.

Awali, daraja hilo lilikuwa likitumiwa kuunganisha mawasiliano ya wakazi wa Gongo la Mboto, lakini wakati wa mvua lilikatika na kusababisha adha kubwa, ujenzi wake ulianza Juni, mwaka huu.

Mratibu wa Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP) Wilaya ya Ilala, Mhandisi Celastina Rwegasira, akizungumzia mradi huo wakati wa ziara ya Bodi ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) jana, alisema mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 4.3.

Alisema awali wakati wa ujenzi wa barabara za Nzimbili zilizoko kwenye mradi wa DMDP, daraja hilo halikuwa katika mpango, lakini baada ya kukata mawasiliano ya wakazi hao, waliamua kuanza kulijenga.

Rwegasira alisema baada ya athari ya mvua mto ulipanuka na kusababisha daraja kusombwa na maji na hivyo wakazi wa eneo hilo wakashindwa kupita.

"Mto ulipanuka na kufikia mita 100 kutoka mita 40 zilizokuwapo, tukaona na hili, ni tatizo kubwa kwa wakazi hawa," alisema Rwegasira.

Aliwahakikishia wakazi wa maeneo hayo kuwa, daraja hilo jipya linalojengwa litaendana na uhalisia wa eneo hilo.

Kuhusu utekelezaji wa mradi ya DMDP Ilala, alisema inatekelezwa kwa fedha za mkopo wa Serikali kutoka Benki ya Dunia (WB) na wako katika kukamilisha awamu ya kwanza ya miaka mitano mwakani.

Alisema katika kipindi cha awamu ya kwanza Halmashauri inatarajia kupokea Sh. bilioni 115 na Sh. bilioni 11.35 zimelipwa kwa wananchi 1,254, kama fidia za kupisha miradi na kati ya fedha hizo Halmashauri imechangia Sh. bilioni mbili na serikali kuu Sh. bilioni 9.35.

Hadi Septemba mwaka huu, alisema halmashauri ilipokea Sh. bilioni 66.69 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa DMDP.

Wananchi wa eneo hilo, waliishukuru serikali kwa kuwaondolea adha hiyo kwa sabbabu wanalazimika kukanyaga maji, ili kuvuka mtu huo.

Mwanaisha Rashid alisema wakati wa mvua wanalazimika kuzunguka umbali mrefu, ili kwenda eneo la jirani na makazi yao kutokana na kukatika kwa daraja hilo.

## Mikoa kunufaika fursa kilimo hai

**Na Faustine Feliciane**

UBALOZI wa Ufaransa nchini kwa kushirikiana na Ubalozi wa Ubelgiji na Shirika la Chakula Duniani (FAO), umeandaa mikutano ya wadau wa kilimo endelevu na wanafunzi wa vyuo katika mikoa ya Morogoro na Arusha.

Ubalozi huo umemleta nchini mtaalamu wa kimataifa wa masuala ya kilimo endelevu kutoka chuo cha AgroParis Tech cha Ufaransa, Prof. Marc Dufumier, ambaye atakutana na wadau wa kilimo endelevu pamoja na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na wale wa Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Nelson Mandela cha Arusha.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Balozi wa Ufaransa nchini, Federic Clavier, alisema Prof. Dufumier atakutana na wadau wa kilimo endelevu kutoka asasi zisizo za kiserikali na za kiserikali pamoja na wanafunzi wa vyuo hivyo, ili kuangalia vikwazo vya kilimo endelevu nchini.

"Hizi ni juhudi za Ufaransa katika kuendeleza kilimo endelevu kama ambavyo wenzetu wa FAO na Ubelgiji wamekuwa na sisi. Tunaamini kilimo endelevu ndiyo njia sahihi ya kuzalisha chakula kwa wingi na utunzaji wake," alisema Balozi Clavier.

Alisema mikutano hiyo itafanyika Oktoba 13 mkoani Arusha na itafanyika mikutano miwili kwa siku chuoni Nelson Mandela. mkutano mwingine utafanyika SUA, Morogoro, Oktoba 16, mwaka huu.

Mkurugenzi wa FAO nchini, Stephen Kargbo, alisema ni vyema kwa Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla kuweka mkazo kwenye kilimo endelevu kwa kuwa ndiyo njia sahihi ya uhakika wa chakula.

Alisema FAO inaunga mkono kilimo endelevu na kwa kushirikiana na wadau wengine, wamekuwa wakisaidia programu mbalimbali za kilimo endelevu kwa maendeleo ya Tanzania, Afrika na dunia kwa ujumla.

Aidha, Balozi wa Ubelgiji nchini, Peter Van Acker, alisisitiza umuhimu wa Tanzania kuendeleza kilimo endelevu kwa kuwa ni njia pekee ya kutunza ardhi kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho.

# Mgombea aahidi ujenzi madarasa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MGOMBEA Ubunge Jimbo la Kibaha Mjini kwa tiketi ya ACT Wazalendo, Aminata Mshana, amesema endapo atachaguliwa kuongoza jimbo hilo, atasimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule zote pamoja na uwapo wa madawati.

Msangi alitoa ahadi hiyo juzi alipokuwa katika mkutano wa kampeni kata ya Maili Moja mjini hapa huku akijinasibu kuwa atahakikisha hakuna changamoto za elimu upande wa vifaa vya kufundishia na samani zinazohitajika shuleni.

Kuhusu afya, alisema atahakikisha anasimamia mpango wa matibabu afya bure kwa wanawake, wazee na watoto huku akiweka bayana kuwa kila mtaa na kata zote 14 kutakuwapo na wataalamu wa afya wanaozungukia nyumba kwa nyumba kupima afya za wananchi.

Katibu wa ACT Wazalendo Kata ya Maili Moja, Mussa Hazirun, alisema kiongozi yeyote akitaka kuongoza anatakiwa kuwapa watoto lishe bora kwanza kama sera ya chama hicho inavyoelekeza. Naye mgombea udiwani wa chama hicho kata ya Maili Moja, Athumani Lusambi, alisema endapo wananchi watamchagua atazungumza na wadau wenye maeneo wayatoe kwa ajili ya kujenga kituo cha afya na kituo cha polisi katika kata hiyo.

Aidha, Lusambi alisema akichaguliwa kuwa diwani atahakikisha anatumia wahisani katika ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya watoto wenye uhitaji maalumu katika shule za msingi zilizoko katika kata hiyo.

Akiwa katika mkutano huo aliwasihi wananchi kuhudhuria kwenye mikutano ya kampeni na kusikiliza sera za wagombea na si kubaki nyumbani na kushabikia vyama vya siasa.

Mgombea huyo pia aliahidi kusimamia suala la daladala kuingia katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi kutoka na sasa kuishia katika stendi ya Njuweni na wagonjwa na ndugu wanaofika katika hospitali hiyo kulazimika kutumia usafiri wa bajaji

# Wazee 1,400 wapatiwa bima matibabu

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

WAZEE 1,388 katika Halmashauri ya Kahama Mji wa Kahama, mkoani Shinyanga, wamekatiwa bima za afya kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa, ili kuwarahisishia upataji wa matibabu na kuimarisha afya zao.

Mjumbe wa Kamati ya Ufuatiliaji wa Baraza la Wazee wilayani Kahama, Ruth Sodoka, alibainisha hayo juzi wakati akisoma risala ya wazee kwenye hafla ya kujadili changamoto zinazowakabili wazee wilayani hapa.

Alisema moja ya matatizo yanayowakabili wazee wilayani hapa ni ukosefu wa matibabu ya uhakika. Alisema wazee wakienda kutibiwa hospitalini wanaambulia vipimo, huku dawa wakiambiwa wakanunue wakati hawana fedha.

"Halmashauri ya Kahama Mji ina wazee 6,792, wanawake 2,793 na wanaume 3,999. Waliokatiwa bima za afya ni 1,388 idadi, ambayo ni ndogo huku wazee 303 wana kadi za matibabu bure. Tunaomba wadau wa maendeleo, watu binafsi na taasisi za kidini watusaidie kutukatia bima za afya," alisema Sodoka.

Naye Katibu wa Baraza la Wazee wilayani Kahama, Anderson Lyimo, akizungumza kwenye hafla hiyo, aliwataja wadau ambao wamewakatia wazee hao bima hizo kuwa ni Halmashauri ya Kahama Mji (wazee 1,200), Kanisa la Mito ya Baraka (70) na watu binafsi wazee 118.

Baadhi ya wazee ambao wamepatiwa kadi hizo, akiwamo Sada Mkumbi, walishukuru kwa kuwa zitawasaidia kupata matibabu kwa urahisi tofauti na awali walipokuwa wakitoa fedha kununua dawa na wanaokosa fedha wanarudi nyumbani kutumia miti shamba. Mkumbi alisema yeye anaishi na wajukuu zake wane, ambao ametelekezewa na watoto wake na babu yao alishafariki dunia na hana uwezo wa kuwapatia huduma zote.

Alisema bima hiyo itawanufaisha na wajukuu zake kupata matibabu bure ikiwa ina hudumia watu sita kwa kaya moja.

Mgeni rasmi kwenye hafla hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Michael Matomola, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, aliwahakikishia wazee wilayani hapa kuwa serikali itaendelea kuwaboreshea huduma za afya kwa kutenga madirisha yao na upatikanaji wa dawa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto), akiwaongoza wafanyakazi na viongozi waandamizi wa benki hiyo, kuwakaribisha wateja waliofika kupata huduma za kibenki katika tawi la benki hiyo makao makuu, jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa wiki ya huduma kwa wateja. **MPIGAPICHA WETU**

# NBC yapongezwa uwezeshaji wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WIZARA ya Kilimo imepongeza juhudi zinazofanywa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa kuwezesha wakulima kupitia mikopo na bidhaa mbalimbali ikieleza kuwa hatua hizo zitawakomboa wakulima wengi dhidi ya umasikini nchini.

Hayo yalisemwa juzi wakati wa kuhitimisha Maonyesho ya Kwanza ya Kahawa yaliyofanyika mjini hapa na kuhusisha wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo na fedha ili kusherekea Siku ya kahawa Duniani. Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gelard Kusaya, alisema taasisi za fedha zina mchango mkubwa katika kuendeleza sekta ya kilimo kupitia uwezeshaji kwa wakulima na wafanyabiashara kwa njia ya mikopo yenye riba nafuu. Kusaya alisema wizara imefurahishwa sana na huduma ya 'NBC Shambani' na kwamba itakuwa na msaada mkubwa kwa wakulima kufanya kilimo-biashara ili waweze kuona tija zaidi.

NBC Shambani ni huduma maalumu kwa wakulima inayowawezesha kufungua akaunti za vikundi (Amcos) au akaunti ya mkulima mmoja mmoja bila gharama za uendeshaji.

"Mkulima anayetaka kujikita katika kilimo biashara ni lazima awezeshwe katika suala la fedha, mikopo mnayoitoa tunaamini inakuwa na faida kubwa kwa mkulima na mkulima ataweza kuzalisha zaidi," alisema Kusaya.

Meneja wa NBC Tawi la Moshi, Lazaro Mollel, alisema maonyesho hayo yamekuwa na faida kubwa katika kufahamu mahitaji ya wakulima hasa wa zao la kahawai ili kuongeza ubunifu wa bidhaa.

Alisema benki hiyo imeleta huduma maalumu kwaajili ya wakulima iitwayo NBC Shambani ambayo inawawezesha wakulima kufungua akaunti za vikundi (AMCOS) pamoja na akaunti ya mkulima mmoja mmoja bila gharama za uendeshaji.

"Huduma ya NBC Shambani inawalenga wadau wote wa kilimo wakiwamo wasambazaji, wakulima, wauzaji wa pembejeo na pia inatoa fursa kwa wakulima wanaofanya kazi kwenye vikundi vya ushirika (Amcos) kufungua akaunti ya kikundi kufungua akaunti ya pamoja na ya mtu mmoja mmoja ambazo uendeshaji wake ni bure," alisema.

Katika maonyesho hayo, NBC ikabidhiwa tuzo ya mdhamini mkuu wa maonesho hayo ambayo ni ya kwanza kufanyika nchini Tanzania.



## HABARI DODOMA

# Wazalishaji saruji walia kero ya tozo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMPUNI za uzalishaji saruji na mbolea nchini zimeomba tozo ya usafirishaji ambayo inatozwa na wizara tatu itozwe na wizara moja ili kupunguza bei ya bidhaa hizo kwa wananchi.

Kampuni hizo ni Dangote, Twiga, Tanga, Mbeya, Lake, Maweni Limstone na Minjingu ambazo zilikutana jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, kujadili tozo mbalimbali za usafirishaji na ukaguzi.

Wakizungumza katika kikao hicho juzi, wawakilishi wa kampuni hizo walisema tozo ya usafirishaji inatozwa na wizara za madini, kilimo na viwanda na biashara na imekuwa kero kwao na kuiomba Wizara ya Madini, tozo hiyo ielekezwe kwenye wizara moja na tozo ya ukaguzi ifutwe au ipunguzwe.

Mwanasheria Mkuu wa Kampuni ya Saruji ya Mbeya, Emmanuel Salla, alisema maombi yao yalilenga kujadili na kupitia tozo hizo ili wao wapunguze bei ya bidhaa inayokwenda kwa wananchi.

Naye Mkuu wa Fedha wa Kampuni ya Saruji ya Tanga, Isaac Lupokela, alisema kikao hicho kina tija kwao kwa kuwa kimefungua wigo mpana katika kuhakikisha kunakuwa na maendeleo ya viwanda.

"Pongezi kwa serikali kwa kuwa 'supportive' sana. ni mabadiliko makubwa katika taifa tumeyaona na tunapongeza," alisema Lupokea.

Akizungumzia hoja hizo, Prof. Msanjila alisema suala la kutozwa tozo ya aina moja kwa wizara kadhaa, atalishugulikia kwa kukaa na makatibu wakuu wenzake wa wizara husika ili kuona namna ya kutatua na kuondoa kero hiyo.

"Andikeni kwa maandishi mniletee muainishe hizo kero na mimi nitawaita makatibu wakuu wenzangu tutakaa na kujadili,"alisema.

Pia alisema serikali inahitaji wawekezaji ili kusaidia kutoa huduma kwa wananchi hivyo kulipa tozo ni muhimu.

Kuhusu malipo ya tozo kufutwa au kupunguza, Prof, Msanjila alisema serikali haiwezi kuziondoa kwa sababu zimepangwa kwa mujibu wa sheria na zilijadiliwa kwa mapana na wadau mbalimbali na kufikia uamuzi huo.

"Mabadiliko haya yanahitaji mjadala mkubwa na wadau wengi," alisema.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangala (kushoto), akikata utepe kuzindua mkakati wa Kitaifa wa utatuzi wa migogoro baina ya Binadamu na wanyamapori wa mwaka 2020 hadi 2024, jijini Dodoma juzi. Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Aloyce Nzuki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tatizo wasimamizi mali za serikali sasa kuwa historia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Fedha na Mipango, imeanza kuchukua hatua za kutatua uhaba wa wasimamizi wa mali za serikali.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mary Maganga, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kikao kazi cha wasimamizi hao kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara ambacho kililenga kutathmini kazi za idara hiyo na maeneo yanayotakiwa kuboreshwa.

Alisema upungufu wa watumishi wa idara hiyo umechukuliwa kwa uzito na serikali hivyo wataanza kuongezewa nguvu kazi ili wafanye kazi kwa ufanisi.

"Maeneo ambayo yana upungufu mkubwa wa nguvu kazi mtaanza kuona watumishi wakiongezeka kwa kuwa hatua za dhati zimeanza kuchukuliwa,"alisema.

Aidha, alisema miongozo iliyotolewa na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali ikiwa ni pamoja na Mfumo wa Kutunza Kumbukumbu za Mali za Serikali (GAMIS) itasaidia kurahisisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi wenye tija wa kujua na kudhibiti mali za serikali katika maeneo yote nchini.

Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali, Chotto Sendo, aliwahimiza wasimamizi hao kusimamia na kutoa tathmini nzuri kwa mali za serikali zinazofutwa kwa kujiridhisha juu ya uchakavu wake kabla ya kutoa taarifa kwa Wizara kwa ajili ya maamuzi. Alisema idara yake ina jukumu la kubuni sera, kanuni, taratibu na miongozo ya kusimamia mali za serikali, kutoa leseni za udalali, kusimamia vifaa vya kutunzia mali pamoja na ufuatiliaji wa mali chakavu ambazo huondolewa kulingana na sheria na kanuni zilizopo.

Sendo alisema idara yake pia ina umuhimu mkubwa kwa wakuu wa mikoa kuwa na uhakika wa mali wanazozimiliki, hivyo kuwasaidia katika uamuzi mbalimbali wa kiuongozi katika eneo lao la utawala.

# Wanufaika mradi wa maji Ntomoko

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANANCHI wa vijiji vinne vya Wilaya za Chemba na Kondoa mkoani Dodoma, wameanza kunufaika na mradi wa maji wa Ntomoko ambao ulikwama kukamilika kwa zaidi ya miaka 40.

Mradi huo uliasisiwa na Rais wa Awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, ambaye aliweka kambi ya siku 30 kuchimba mfereji wa kusambaza maji, lakini ulisimama kufanya kazi baada ya bwawa lililokuwa likizalisha maji kujaa tope.

Hata hivyo, serikali iliamua kufufua mradi huo kwa kuwekeza Sh.bilioni mbili ambazo zimesaidia wananchi wa vijiji vya Kinkima, Mtakuja, Kilele cha Ng'ombe na Makirinya kupata huduma hiyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, wakazi hao walisema mradi huo umesaidia kuwaondolea tatizo la muda mrefu la kufuata maji umbali mrefu.

Mmoja wa wananchi hao, Hassan Bakari, alisema wananchi wa Makirinya wamefurahishwa na hatua hiyo kwa kuwa inalenga kuwatua ndoo kina mama ambao wamekuwa wakihangaika kutafuta maji kwa muda mrefu vijiji vya jirani.


Alisema awali walikuwa wanachota maji kijiji cha Busi au Kwadero ambapo ni umbali mrefu.

Naye Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mapango, Zuhura Juma, alisema kero ya maji kwa sasa ni historia kwenye vijiji hivyo.

"Hakukuwa na maji kabisa hapa wananchi walikuwa wanatembea zaidi ya kilometa 20 kufuata maji lakini baada ya mradi kukamilika tunatarajia kupata maji safi,"alisema.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Robert Mganga, aliwahakikishia wananchi kuwa watakuwa na uhakika wa maji na kwamba kwasasa mradi upo kwenye matazamio.

"Wananchi watapata maji kipindi chote hiki na tunafanya majaribio kwa mwezi mzima huku maji yakitoka na wakati huo pia tutakuwa tunafanya utaratibu wa namna bora ya kuendesha mradi huu,"alisema.





# Zantel yazindua huduma nyingine

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya simu za mkononi Zantel imezindua Ezy Gazeti, ili kurahisisha maisha ya wateja wao kupitia simu za mkononi na kufaidika na huduma zinazotolewa na mtandao huo.

Akizungumza katika uzinduzi wa huduma hiyo mjini hapa jana, Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohammed Khamis Mussa (Baucha), alisema hatua hiyo ni mfululizo wa mikakati ya Zantel katika kuboresha huduma kwa wateja wake.

Aidha, alisema hatua hiyo pia itatoa suluhisho la kidijitali litakaloziba pengo la upatikanaji wa habari muhimu kwa kuwasaidia watu kusoma magazeti kutumia simu zao za mkononi popote walipo hasa katika maeneo ya vijijini.

Alisema lengo la kuzindua huduma hiyo ni kuwapa fursa wateja kupitia simu zao kuona wanapata magazeti wanayotaka kila siku na kusoma taarifa mbalimbali zinazotokea nchini Tanzania.

Baucha alisema magazeti pia, yanaweza kutumika kupata kumbukumbu za nyuma katika magazeti yake hivyo hatua hiyo ni muhimu kwa mtandao huo katika kuimarisha maisha ya watu.

Hata hivyo, alieleza kwamba lengo la mtandao huo ni kuhakikisha inatoa huduma mbalimbali, ili ziweze kuwarahishia wateja wake.

"Zantel tupo kwa ajili ya kutoa huduma siku 365 kwa mwaka na kuona zinawafikia wananchi wote, ambao wanatumia mtandao huu," alisema.

Alisema Zantel iko katika mkakati wa kuona mikopo wa wanafunzi inalipwa kwa kutumia Ezypesa na hata wakulima wa karafuu wanalipwa kwa kutumia huduma hiyo na Shirika la Biashara za Zanzibar (ZSTC).

Sambamba na hayo, alisema Zantel imejipanga kutoa huduma za kidijital na kuona wateja wote wanakwenda sambamba na mfumo huo.

Naye, Meneja Biashara wa Ezy Gazeti Tanzania kutoka kampuni ya 'Smart Code' Johahhes Julias Lutachalwa, alisema wameungana na Zantel, ili kuwa na teknolojia, ambayo itaweza kuwarahisishia wateja wao kupata taarifa mbalimbali kiganjani.

Alisema hatua hiyo pia itarahisisha watu kupata taarifa mbalimbali ndani na nje ya nchi, ili kupata taarifa mbalimbali kupitia magazeti yanayochapishwa Tanzania. Pia alisema mteja anaweza kuweka kumbukumbu kwa gazeti lake katika simu yake na kusoma wakati wowote.

# Wazazi kikwazo kesi za ukatili kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Dawati la Jinsia Wanawake na Watoto kutoka Jeshi la Polisi Makao Makuu Zanzibar, Suleiman Haji Hassan, amesema moja ya vikwazo wanavyokabiliana navyo katika kesi za udhalilishaji wa kijinsia ni ushirikiano mdogo kati yao na wazazi wa waathirika wa vitendo hivyo.

Suleiman aliyasema hayo jana katika mkutano wa wadau wa malezi, ulinzi na usalama wa mtoto uliofanyika mjini hapa ikiwa ni miongoni mwa harakati za kuekelea Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika.

Alisema baadhi ya wazazi wanapotakiwa kutoa ushahidi au msaada mwengine, ili kufanikisha kesi kufikia mahali pazuri, huwa wagumu kutoa ushirikino.

Ofisa huyo alisema licha ya dawati kupokea malalamiko hayo, hawawezi kuyafikisha katika hatua zaidi za kisheria kama hajamaliza ujazaji mjalada ikiwamo ushahidi dhidi ya matukio hayo kwa watu wa karibu.

Meneja Utetezi kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Salma Lusangi, alisema matukio 649 ya ubakaji watoto wa kike wenye umri chini ya miaka 18, yameripotiwa katika vituo mbalimbali vya polisi Zanzibar kuanzia Januari, mwaka jana, hadi Agosti, mwaka huu.

Alisema kati ya matukio hayo, manne tu ndiyo yaliyopatiwa hatia na kesi 370 ziko chini ya upelelezi na 123 ziko mahakamani.

Lusangi alisema kesi 88 zimefungwa na Jeshi la Polisi na 48 ziko Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashataka (DPP) huku kesi 16, wahusika wakiwa wameachiwa huru.

Hata hivyo, Lusangi alisema kwa upande wa matukio ya ulawiti, 147 yameripotiwa katika kipindi hicho na ni kesi moja tu iliyopata hatia.

Alisema kesi 93 ziko chini ya upelelezi, kesi 15 zimefungwa, kesi sita ziko ofisi ya DPP na 22 ziko mahakamani.

Naye Ofisa kutoka ofisi ya DPP, Sabra Machano Khamis, alisema licha ya kupokea majalada mengi kutoka polisi, lakini hawawezi kuyafikisha mahakamani kutokana na ukosefu wa masuala ya kisheria.

Alisema baadhi ya wazazi wanapotakiwa kukamilisha taratibu hizo huwa wagumu kufika na kutoa maelezo, jambo ambalo linajitaji nguvu ya pamoja katika kulimaliza.

Akifungua mkutano huo, Kaimu Mkurugenzi wa Kijiji cha Kulelea Watoto walio kwenye Mazingira Magumu, Asya Maulid, alisema juhudi za msingi zinahitaji kuchukuliwa, ili mtoto wa kike kupata mahitaji muhimu ikiwamo elimu.

Alisema baadhi ya vitendo vya udhalilishaji, zikiwamo mimba na ndoa za mapema, vinachagia kumkosesha mtoto wa kile kupata haki ya msingi ya elimu.




Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale wa Zanzibar, Mahmoud Thabit Kombo, akitoa fedha kwenye ATM za benki ya NMB kwa kutumia kadi ya UnionPay, kuashiria uzinduzi rasmi wa ushirikiano kati ya benki hiyo na UnionPay International (UPI), katika hafla iliyofanyika mjini Zanzibar juzi. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi (kulia) na Meneja wa benki hiyo, Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kadi za UnionPay kutumika ATM za NMB

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI ya NMB na Kampuni ya UnionPay International (UPI), zimeingia makubaliano yatakayowezesha kadi za malipo za UnionPay kuanza kukubalika katika kufanya miamala kwenye mashine za kutolea fedha (ATM) na zile za kufanyia ununuzi (POS) za NMB.

Kampuni hizo pia zimezindua jukwaa la biashara litakalowezesha wafanyabiashara kufanya miamala kupitia tovuti zao (E-Commerce Platform) katika hafla iliyoongozwa na Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mahmood Thabiti Kombo.

Akizungumza katika hafla hiyo juzi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema kwa uzinduzi huo, wafanyabiashara na kampuni za huduma zitawezeshwa kupokea malipo kimtandao kupitia tovuti zao, bila ulazima wa wateja kutembelea sehemu za biashara zao.

Zaipuna alisema ushirikiano na UPI utaleta unafuu na uharaka wa kufanya miamala kwa watumiaji wa kadi za UPI watakaokuwa wanapata huduma kwenye mtandao wa ATM na POS wa NMB muda wowote.

"Hii ni hatua muhimu sana katika kuleta huduma bora kwa wateja wetu, ni fursa pia kwa wafanya biashara hasa wa sekta ya hoteli, maduka, na utalii kwa ujumla katika kuwezesha biashara ya kimataifa kupitia malipo mtandao yanayowezeshwa na benki ya NMB," alisema.

"Kwa mtandao wetu wa zaidi ya POS 1,750 POS na ATM zaidi ya 800 nchini, huduma hii inategemewa kuleta mapinduzi katika matumizi ya kadi kwa watumiaji wa UnionPay," aliongeza.

Naye Meneja Mkuu wa UPI, Luping Zhang, alisema kadi za kampuni hiyo zinajulikana kama nyenzo muhimu ya malipo kwa kufanikisha biashara, utalii na mwingiliano wa kiutamaduni kati ya bara la Afrika na Asia.

"Ushirikiano huu kati ya benki ya NMB na UnionPay International utaongeza matumizi ya kadi za UnionPay nchini na katika miamala ya kimataifa na inaashiria mapinduzi ya teknolojia ya malipo kupitia kadi," alisema na kuongeza:

"Tuna furaha kushirikiana na benki kubwa ya NMB kuleta huduma hii muhimu kwa sekta ya utalii Tanzania."

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Kombo alisema nchi za Bara la Asia hutoa watalii wapatao milioni 250 kwa mwaka.

"Tukipata asilimia moja tu ya hawa basi tuko vizuri kwani itakuwa ni zaidi ya watalii wote walioitembelea Zanzibar kwa mwaka jana," alisema.

Mwaka jana, Zanzibar ilipokea watalii 538,425, ambao walileta fedha za kigeni zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 421.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI OKTOBA 10, 2020



DAVIDO SASA UNATAKA UBUNGE? Uk.14



# HIYU NDIYE DIAMOND

# Ukimshika mguu, atakuachia kiatu

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Naseeb Abdul, maarufu kama Diamond Platnumz, hivi karibuni ameishtua dunia baada ya waandaaji wa tuzo za Grammy, kumtaja kama taswira ya muziki wa Afrika Mashariki.

Katika mtandao wao wa @recordingacademy, timu ya waandaaji wa tuzo hiyo kubwa duniani, wamesema kijana huyo wa Kitanzania amechangia lugha ya Kiswahili kuanza kutamba katika muziki wa Marekani.

Baadhi ya wanamuziki wa Marekani ambao Diamond amefanya nao kazi ni, Omarion, Rick Ross, Ne-Yo na Alicia Keys.

Baadhi ya wachambuzi wa muziki wamesema kutajwa pekee katika mtandao huo ambao mastaa wengi duniani wanatamani, ni jambo la kujivunia na kwamba limeleta matumaini siku moja msanii huyo atatajwa katika majina ya wasanii watakaowania tuzo hizo.

"Tuzo za Grammy ni maarufu duniani na kila msanii anataka kutajwa ili kupandisha soko lake, suala la kuhojiwa kwa Diamond inatosha kutupa matumaini siku moja ataingia katika kinyang'anyiro," amesema Shukuru Mkenge.

Aidha, kupata nafasi ya kuhojiwa katika mtandao huo ni kama anasafishiwa njia kuelekea katika soko lingine la kimuziki, hasa kutokana na mchanganyiko wa lugha mbili za Kiswahili na Kingereza kuwa kivutio.

Anashauriwa kutovimba kichwa kwa mafanikio anayopata, badala yake aendelee na ubunifu katika kazi zake na siku moja ataweza kuliweka jina la Tanzania, katika orodha ya juu kimataifa.

## BASI SAWA

## Harmonize kadokeza hili...

KUNA Kila dalili, mwanamuziki wa Bongo Fleva, Harmonize, yupo mbioni kukamilisha albamu yake ya pili ambayo inawezekana ikaitwa 'High School'.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram Harmonize amedokeza kwa kuposti picha akionekana yuko studio na kisha aliandika ujumbe usemao 'High School Albam. Mwaka huu Harmonize, aliachia album yake ya kwanza iliyoenda kwa jina la Afroeast, ambayo aliwashirikisha wasanii tofauti tofauti.



## Dudu Baya katoweka nyumbani

MSAKO wa kumtafuta mwanamuziki wa siku nyingi, Godfrey Tumaini, maarufu kama Dudu Baya, umeanza siku moja baada ya mtoto wake kutangaza ametoweka.

Kupitia ukurasa wa Instagram, binti wa msanii huyo, anayejulikana kwa jina la Maria, amethibitisha kuwa baba yake ametoweka tangu tarehe 13 mwezi uliopita na hajulikani aliko.

Dudu Baya ambaye amejizolea umaarufu kutokana na tabia yake ya utata, hajulikani aliko na katika ukurasa wake wa Istagram, alionekana kuposti agosti 12 kwa kuandika ujumbe kuwa watu watarajie kusikia kitu kizito.






## Jaydee kabanwa mbavu

MWANAMUZIKI mkongwe, Lady Jaydee, amebanwa na serikali baada ya kutakiwa kufafanua wimbo wake mpya ambao unadaiwa kuhamasisha matumizi ya bangi.

Kaimu Ofisa Habari wa Baraza la Sanaa Tanzania (Basata) Godfrey Nago, amekiri kumtumia barua ya wito Lady Jaydee, ili akafafanue maana halisi ya wimbo huo.

"Tumemuita yeye kwanza na tayari tumeshampelekea barua kupitia mwanasheria wetu ambayo anatakiwa aripoti hapa, halafu kuanzia hapo ndiyo tutakuwa na cha kuzungumza naye, huwezi kutoa hukumu kabla hujamzikiliza mtu"



## Vanessa yu hoi taabani

MAPENZI mubashara! Ndivyo msanii wa muziki wa kizazi kipya, Vanessa mdee, amejikuta akizidi kuelemewa na mahaba mazito ya mpenzi wake Rotimi.

Wawili hao sasa wameamua kuonyeshana mahaba niue kwa kila mtu baada ya kuchorana michoro ya tattoo yenye majina yao kwenye miili yao.

Kupitia video ambazo zimesambaa katika mitandao ya kijamii, zimewaonesha kila mmoja kamchora Tattoo mwenzake ikiwa kama ni ishara ya upendo na kumbukumbu.



## Majina yao ya utani yalianzia hapa

**Na Adam Fungamwango**

MAJINA ya utani si jambo la ajabu kwa watu wengi maarufu duniani. Wanamuziki, wasanii na wanamichezo wengi duniani pamoja na kwamba wamekuwa na majina yao halisi, lakini wengine wamekuwa wakijulikana zaidi kwa majina yao ya utani, wakati mwingine kufunika kabisa yale halisi.

Lakini mara nyingi majina ya utani hayazuki tu, badala yake kuna mahali yanaanzia. Wakati mwingine inakuwa kama mzaha tu, tayari ndiyo linakuwa jina.

Sitaki hapa kueleza jinsi Kizota na Tashabalala walivyopata majina hayo, ila leo nikajikita kuelezea jinsi yalivyopatikana majina ya utani ya wanamuziki wa dansi.

**MOSHI WILLIAM 'TX'**

Ukitaka kulitaja jina lake ni lazima uanze na Tx Moshi William. Huyu alikuwa ni mwimbaji maarufu na mtunzi wa bendi ya Msondo Music aliyefariki mwaka 2006 jijini Dar es Salaam.

Alipewa jina la TX na mtangazaji wa Redio Tanzania wakati huo, marehemu Julius Nyaisanga.

Mwaka 1982, alihamia Msondo akitokea Polisi Jazz Band. Na wakati huo kuna magari wa wataalam kutoka nje ya nchi yalikuwa wakisajiliwa kwa kuanzia neno TX, halafu namba za magari kama vile TZ au T kwa sasa.

Moshi alionekana ni kama mtaalamu kutoka Polisi aliyeingia Msondo, ndipo akapachikwa jina la TX, likawa kama jina lake halisi.

**ATHUMANI MOMBA 'SAUTI YA CHUMA'**

Alikuwa mwimbaji wa bendi mbalimbali kama Vijana Jazz, Bima Lee na alifariki mwaka 2005 akiwa kwenye bendi ya Msondo Ngoma Music.

Huyu alipewa jina la 'Sauti ya Chuma' kutokana na sauti yake kuwa kali na ya juu.

Hayati Hemed Maneti ndiye aliyempa jina hilo wakati akiwa Vijana Jazz. Ni wakati wa mazoezi, alipewa wimbo mmoja auimbe. Aliuimba kwa sauti kali na ya juu, kiasi kwamba Maneti akacheka na kumwambia "Mhh punguza kidogo, maana hiyo sauti kama chuma." Kuanzia hapo akaanza kuitwa 'Sauti ya Chuma.'

**JERRY NASHON 'DUDUMIZI'**

Huyu alikuwa mwimbaji wa bendi za Vijana Jazz na Bima Lee. Alifariki mwaka 1995. Alikuwa na sauti nzito na yenye kitetemeshi. Awali alipojiunga na vijana kutoka Magereza Jazz alikuwa akipiga 'gitaa la rhythm.' Wakiwa safariki Maneti alipatwa na mafua, hivyo akataka msaidizi, kwani asingeweza kuimbisha na kuitikia, hivyo alimtaka mmoja amsaidie. Kwa sababu Nashon aliweza, alimsaidia. Jinsi alivyoimba, ilimpendeza sana Maneti akamwambia "Wewe inaimba kama Dudumizi." Kuanzia hapo jina lake likawa Dudumizi, na ndipo rasmi alipoanza kuimba na kutunga hadi anafariki dunia.

**ROGART HEGA 'KATAPILA'**

Labda watu wanaweza wakadhani kuwa hilo lilitokana na mambo ya muziki, la hasha. Ni kwamba kwenye miaka ya '90 wakati Hega alianza muziki akiwa na bendi za Washirika Tanzania Stars kulikuwa na viatu aina ya 'caterpillar' ambavyo vilikuwa ndiyo vinaingia nchini. Mwanamuziki huyo alikuwa mpenzi mkubwa wa kuvaa mdundo huo, kiasi cha wenzake kumpachika jina hilo.

**MOHAMED SALUM 'GOTAGOTA'**

Alikuwa mwimbaji wa bendi za Tabora Jazz, Mwenge Jazz na hatimaye Vijana Jazz. Alifariki katikati ya miaka ya 1990.

Kutokana na sauti yake kuwa tamu, mashabiki waliifananisha na ndege anayegonga kwenye miti, aitwaye 'gotagota'.

## Siri Yangu; Ngoja ngoja huumiza matumbo

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine methali za Kiswahili zinajipinga zenyewe kutokana na mazingira ya matukio. Mfano unaambiwa 'subira yavuta heri', lakini hapo hapo kuna nyingine inayoipinga inasema 'ngoja ngoja huumiza matumbo'.

Na kuna wakati kama kuna kitu unakitaka au kinakutatiza ni bora useme tu badala ya kusubiri au kukaa na siri moyoni. Siri hii ninayoisema ni ile ambayo ukiisema inaweza ikakusaidia, lakini mtu anashindwa kuisema tu kwa kuona aibu au kuona sijui ataeleweka nini kwenye jamii.

'Siri Yangu' ni filamu inayoonyesha makosa ambayo baadhi ya jamii inayafanya. Mtoto wa kike siku zote anaambiwa yeye ndiye anayetongozwa na si kueleza hisia zake. Wakati mwingine matokeo ni mabaya kuliko inavyotegemewa.

Imechezwa na wasanii wengi, baadhi yao wakiwa ni Robert Kassim, Said Real, Hadija Maksimo, Jasmin Gagu, Hamida Mbwana, Zakia Mussa, na Dhakra Mbiza.

Said ni kijana anayeishi kijijini, akijishughulisha na kilimo akiwa mmoja wa wanakijiji vijana mwenye heshima na adabu.

Hii inamfanya kupendwa na watu wote, wakubwa, wadogo, wazee, vijana na akinamama. Hata akidada nao walimpenda. Kwa hao akinadada wapo waliompenda kimapenzi.

Mmoja wapo ni Asumina. Asumina na Said wamekuwa hapo kijijini kwa muda mrefu. Asumina alikuwa akimpenda Said na kuumia moyoni, lakini alishindwa kumwambia kwa utamaduni ule ule na mtoto wa kike hawezi kumuanza mtoto wa kiume. Lakini Bishura alishindwa hata kujiongeza basi, amtege ili Said aingie. Badala yake alikuwa akiumia na siri moyoni mwake.

Bisura, msichana aliyetoka mjini na kuhamia kijijini hapo baada ya kumaliza shule, alimuona Said, akampenda.

Baada ya kukaa muda na kuzoea mazingira ya pale, akaona isiwe tabu. Akaandika barua kuonyesha ni jinsi gani anavyompenda Said. Kwanza Said alitafakari. Baada ya ushauri kwa rafiki yake, akakubali. Mapezi kati yake na Bisura yakaanza. Ni mapenzi motomoto. Mapenzi nayo hayana siri na siri si ya watu wawili. Asumina akajua hilo. Roho ikamuuma. Kiguu na njia kwa mganga na kienyeji kuroga ili penzi livunjike. Haikuwa hivyo. Penzi la Said na Bisura lilikwenda hadi ikawa ndoa. Siku ya ndoa, Asumina akaanguka na kufariki dunia na inagundulika amekunywa sumu, lakini sababu hakuna. Mwaka mmoja baada ya harusi kufungwa na pia msiba wa Asumina, ndipo Said alipomwambia mkewe siri. Alimwambia kumbe alijiua kwa sababu alimpenda lakini alishindwa kumwambia. Mke akamuuliza alijuaje, akasema wakati wanamkagua alikutana na karatasi iliyoandikwa maneno hayo, lakini alishindwa kuitoa mbele za watu kutokana na mazingira kutokuwa rafiki wakati huo na kumtaka mkewe pia kufanya siri.

Wakati huo tayari Asumini ni mjamzito. Wote wakakubaliana mtoto akizaliwa wa kiume aitwe Asumani, kama wa kike aitwe Asumina kwa ajili ya kumbukumbu na msichana huyo aliyempenda Said lakini akashindwa kumwambia, hadi msichana kutoka mjini alipokuja na kuchangamkia tenda.





# Nicki Minaj hongera yako

HATIMAYE rapa wa Marekani, Nicki Minaj, na mume wake Kenneth Petty, wamepata mtoto wa kwanza katika ndoa yao.

Kulingana na mtandao wa TMZ, wawili hao walimkaribisha mtoto wao siku ya Jumanne iliyopita, baada mwezi Julai mwanamuziki huyo kuthibitisha kwamba ni mjamzito.

Wanandoa hao bado hawajatoa tamko rasmi, lakini taarifa zinadai tayari wamepata mtoto na wanajiandaa kumtambulisha kwa mashabiki wao.



## Chacha subiri watu waanze mistari

MSANII nyota wa filamu Nigeria, Chacha Eke, ametangaza ndoa yake na Austin Faan, iliyodumu kwa miaka saba imevunjika.

Mwigizaji huyo aliposti video fupi katika mitandao ya kijamii, akielezea mwisho wa ndoa yake na kuwataka mashabiki wake kutofadhaika.

"Unaweza kusema nimechanganyikiwa, lakini si hivyo. Video hii inaweza kuiambia Dunia kwamba ndoa yangu imekwisha fika ukingoni. Hakuna sababu ya uthibitisho, ni kwamba tumeachana na mwanamume huyu," ameandika.

## Davido sasa unataka ubunge?

MWANAMUZIKI wa Nigeria, David Adeleke, maarufu kama Davido, amesema anafikiria kugombea nafasi ya ubunge siku zinazokuja.

Staa huyo wa muziki, alikuwa akitumiana ujumbe na Ebuka Obi-Uchendu, ndipo alipoelezea kuwa na ndoto ya kuwania nafasi hiyo ya kisiasa.

"Nitaanza kama mjomba wangu, ilikuwa mara ya kwanza kujiunga na familia yangu kugombea kwenda ofisini," ameandika Davido.





## Regina mbona unataka kulikoroga

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Regina Daniel na mumewe bilionea Ned Nwoko, wamewashtua mashabiki wao baada ya kila mmoja kumfuta mwenzake katika ukurasa wa Instagram.

Tukio hilo ambalo limewashangaza wengi, limesababisha mjadala mkali katika mitandao ya kijamii, huku baadhi wakidai kuna dalili wawili hawapo vizuri na muda wowote watatangaza kuachana.

Lakini haijkuwekwa wazi kwa nini wanandoa hao wameamua kuondoana Istagram, wakati walikuwa na maisha mazuri.

## Lil Frosh mapenzi si kipigo bhana

MPENZI wa rapa kutoka Nigeria, Lil Frosh, amefunguka akidai alishambuliwa usoni na msanii huyo.

Gift Camille, ambaye alikuwa mpenzi wake, akitumia ukurasa wake wa Twitter, ameandika kwamba shambulio hilo lilimsababishia maumivu na kwamba anajuta kuwa karibu na mwanamuziki huyo.

"Nafahamu kwamba ningesema haya mwanzo, ameharibu sura yangu frosh wakati wa uhusiano wetu takribani miezi kumi sasa," ameandika.






MAKALA

# SIMULIZI LA MWENYE ULEMAVU (1)

## ■Nilikosa chanjo nikapata polio, upofu
## ■Ushirikina ukazidi kukoleza matatizo

**Na Mwandishi Wetu**



Eligius Bwalya akiwa kazini ofisi za Baraza la NECTA Dar es Salaam. **PICHA: MWANDISHI WETU**

NAITWA Eligius Bwalya, nilizaliwa Julai, 06, 1986 katika Kijiji cha Muzi kandokando ya ziwa Tanganyika Wilaya ya Sumbawanga Vijijini ambayo leo inaitwa Kalambo mkoani Rukwa.

Nikiwa mzima na viungo timamu mama yangu alinipokea kwa furaha zote kutoka kwa wakunga , nikiwa mtoto wa saba katika familia ya mama Augustino Mbao na Simon Bwalya, iliyokuwa na watoto 10.

Wanawake sita na wanaume wane ndugu zangu wawili wamefariki dunia. Namshukuru Mungu kuwa mimi peke yangu ndiye niliyebahatika kusoma, ndugu zangu wengine ambao wengi wao waliishia darasa la saba.

**MWANZO ULEMAVU**

Nilizaliwa mzima lakini changamoto ya ulemavu ilianza nikiwa na miaka minne mwaka 1990 baada ya kuugua polio au pepopunda iliyosababisha nipate ulemavu baada ya mguu mmoja kukosa nguvu na kushindwa kufanyakazi nikianza kutumia gongo kutembea.

Kutokana na kuwapo kwa mila, desturi na Imani za kishirikina katika jamii zetu, wazazi wangu waliamini kuwa ulemavu umetokana na kurogwa japo hospitalini ilionyesha kuwa nina tatizo la polio.

Chanzo cha ulemavu ni wazazi wangu kushindwa kunipeleka hospitalini kwenye chanjo zinazotolewa kwa watoto ili kuwakinga na magonjwa mbalimbali ukiwamo huo wa polio.

**ULEMAVU WA MACHO**

Niliendelea na ulemavu wa mguu hadi nilipoanza safari yangu ya elimu, Januari 1993 ambapo nilianza darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Muzi iliyopo katika Kijiji cha Muzi, nilisoma miezi mitatu tu na matatizo ya macho yakaanza.

Safari hii niliugua surua ugonjwa ulinishambulia macho na kuniacha na upofu. Hali kadhalika, katika suala hili la ulemavu wa macho bado wazazi wangu waliamini kuwa kuna mkono wa mtu ambaye kwa mujibu wa imani yao mtu huyo alitaka kuvuruga na kuharibu kabisa kipaji changu kwani nilionyesha dalili kuwa nina uwezo, kipaji na akili nyingi na pengine ningefika mbali.

Vipimo hospitalini vilionyesha kuwa tatizo la macho yangu lilitokana na ugonjwa wa surua na chanzo ni kutokuwa na chanjo ambayo huwa ni kinga ya utotoni kama nilivyoikosa kwenye pepopunda na kusababisha niugue polio.

Ninaishi na ulemavu mkubwa wa aina mbili, yaani macho na viungo. Kutokana na mkanganyika juu ya nini kilisababisha kuwa hivi nilivyo, bado ninaamini kuwa yote hayo yalitokana na mipango ya Mungu kwa kuwa tunafundishwa katika imani kuwa kila kinachotokea duniani, Mungu ameruhusu.

Nilipata matibabu na baadaye nikaanza kuona tena japo ulikuwa ni uoni hafifu (low vision). Niliishi na hali hii kwa miaka mitano mpaka nilipopelekwa kuanza shule Machi, 1998.

Shule hiyo ilikuwa katika Kijiji cha Kaengesa wilayani Sumbawanga mkoni Rukwa. Miaka hiyo Shule ya Msingi Kaengesa ilikuwa inajumuisha wanafunzi mchanganyiko wasioona na wasio na ulemavu.

Nakumbuka shuleni nilipokelewa na walimu m Revokatus Mlyato (sasa ni marehemu) na mwezake Conorald Ndenje. Shukrani nyingi zimwendee asiyeona mwenzangu, Bathlomeo Ntinda ambaye ndiye aliyenipeleka shule kwani wakati huo alikuwa mwenyekiti wa chama cha wasioona (TLB) mkoa wa Rukwa.

Nilisoma hapo kwa muda wa miezi mitatu na tulipofunga shule kwa ajili ya likizo ya Juni, nilirudi nyumbani kwa mapumziko.

**KUONDOLEWA JICHO**

Wiki mbili kabla ya kufungua shule, nilianza kuugua macho tena hadi nikafanyiwa oparesheni ya jicho katika hospitali ya Mkoa wa Rukwa ili kuokoa maisha ilibidi kuondolewa jicho moja kwani kulikuwa hakuna namna ya kuona tena.

Huo ulikuwa mwezi Agosti 1998 na nililazwa hapo hospitalini kwa zaidi ya mwezi mmoja na nilipopona, tayari shule maalumu ya wasioona ilikuwa imekamilika kujengwa mjini Sumbawanga eneo la Malangali.

Shule hii ilijengwa kwa msaada wa Wajerumani kupitia Padre Luka, ambaye ni Mjerumani. Wakati natoka hospitalini nikakuta shule hii imefunguliwa rasmi na Rais wa awamu ya tatu wa Benjamin Mkapa, alipokuwa ziarani Rukwa mwaka 1998.

Kwa kuwa mpaka nafumba macho nilikuwa tayari nilishajua kusoma maandishi ya wasioona na kwa kuwa nilikuwa na uwezo mkubwa kitaaluma, hata nilipotoka hospitalini, nilirushwa darasa moja nikaanza darasa la pili; na kwa sababu hiyo nikasoma madarasa mawili ndani ya mwaka mmoja wa 1998.

Nikiwa shuleni Malangali, niliwahi kuwa kiranja mkuu kwa miaka minne tangu mwaka 2000 mpaka 2003.

**KIFO CHA BABA**

Licha ya kupitia changamoto nyingi nilizopata nilikuwa nasaidiwa na wazazi baba na mama. Nikiwa darasa la saba Juni 2003, nilipata pigo la kuondokewa na baba yangu mzazi aliyefariki dunia kutokana na kiharusi (stroke attack).

Hali hii ilinifanya nitetereke kisaikolojia japo niliendelea na harakati za kupata elimu.

Septemba 2003 nilihitimu elimu ya msingi ambapo na Januari 2004 nilichaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari katika Sekondari ya Kantalamba iliyopo katika Manispaa ya Sumbawanga.

**SAFARI YA SEKONDARI**

Shule hii nayo ilikuwa inajumuisha wanafunzi mchanganyiko. Nikiwa shuleni Kantalamba, nilipenda kushiriki katika matukio mbalimbali yaliyokuwa yakitukia shuleni hapo kwa mfano mahafali, mijadala na hotuba mbalimbali zilizotakiwa kutolewa na mwanafunzi.

Kutokana na ushiriki wangu katika matukio mbalimbali nilijikuta nimepewa jina la "promoter". Lilijulikana kiasi kwamba likafunika jina langu halisi na mpaka sasa ndilo jina ninalofahamika mno miongoni mwa watu wote waliowahi kukutana na mimi kwa namna moja ama nyingine katika harakati za masomo.

Pia nikiwa Kantalamba, niliwahi kuwa kiongozi mwakilishi wa wanafunzi wenye uhitaji maalumu na mnamo mwaka 2007 nilihitimu kidato cha nne na matokeo yalipotoka nikapata daraja la tatu la 3.22.

Matokeo haya yaliniwezesha kuendelea na kidato cha tano Aprili 2008 katika shule hiyo hiyo ya sekondari Kantalamba kwa mchepuo wa masomo ya Sanaa nikisoma Historia, Kiswahili na Kiingereza (HKL).

**CHUO KIKUU UDSM**

Ilipofika Februari 2010, nilihitimu kidato cha sita, na safari hii nilipata daraja la kwanza (division 1.9) ambapo mwaka huo huo mwezi Oktoba nikajiunga na elimu ya juu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nikiwa chuoni hapo, nilisoma shahada ya kwanza ya elimu ya watu wazima na maendeleo ya jamii (Bachelor of Education in Adult and Community Education).

**CHANGAMOTO UDSM**

Kutokana na aina yangu ya ulemavu, mazingira ya Chuo Kikuu UDSM yalitaka kuwa kikwazo kwangu katika safari ya masomo chuoni hapo. Hii ni kutokana na hali halisi ya mazingira na miundombinu yake kuwa na maghorofa na ngazi nyingi. Vilevile mtindo wa kusoma huku unakimbizana na vipindi kutoka jengo moja kwenda jingine ilielekea kunikwaza na kutishia mustakabali wa masomo yangu.

**BAJAJI ILININUSURU**

Hata hivyo changamoto hizo ziliondolewa. Kutokana na mipango na sera ambazo chuo kilikuwa kimejiwekea, changamoto hizo zilitatuliwa kwa kununuliwa pikipiki ya magurudumu matatu (bajaji) ambayo nilipewa dereva na mafuta ya lita tano kila wiki.

Suala hili lilinifanya nisome kwa utulivu na changamoto zilizobaki niliweza kuzimudu. Shukrani nyingi ziwaendee waliyokuwa katika kitengo cha elimu maalumu kwa wakati huo wakiongozwa na Nsimbila, Jerome Mbago na na Profesar Mfinanga na aliyekuwa mshauri wa wanafunzi Dk. Martha Koro.

Wote hawa walichangia pakubwa katika masomo yangu. Nikiwa chuoni hapo, niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Walemavu (DUHA) na mbunge wa bunge la wanafunzi (USRC) tangu mwaka 2011 mpaka 2012.

**ITAENDELEA**

MAKALA

# EWURA ilivyopania kutokomeza vishoka umeme kila kona ya nchi

Na Augusta Njoji, DODOMA



Fundi akiunganisha umeme nyumbani. Sheria ya Umeme inataka mafundi wa namna hii wawe na leseni na vyeti vinavyotambulikana. **PICHA: MAKTABA.**

BILA umeme hakuna viwanda na bila umeme maisha ni magumu. Kutokana na ukweli huo, serikali imeweka mkakati kuhakikisha ifikapo mwaka 2021, umeme uwe umefika kila nyumba nchini.

Kutokana na umuhimu wa nishati hiyo kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, serikali imekuwa ikitekeleza miradi ya umeme vijijini.

Hivi karibuni, Rais John Magufuli, akieleza mafanikio yaliyopatikana chini ya serikali ya awamu ya tano, anasema kwa kipindi cha miaka mitano serikali imepeleka umeme katika vijiji 9,402.

"Tulipoingia madarakani ni vijiji 3,000 tu ndio vilikuwa na umeme Tanzania nzima, katika kipindi cha miaka mitano tumepeleka umeme vijiji vimefika 9,700,na sasa vimebaki vijiji 2,500 ambavyo hadi kufikia Juni 2021 vitakuwa vimefikiwa na umeme,"anasema.

Pia anasema ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere katika Mto Rufiji ambao utakuwa na uwezo wa kuzalisha Megawati 2, 115 utaifanya Tanzania kuwa na umeme wa kutosha.

Pamoja na utekelezaji wa azma hiyo, kumekuwapo na wimbi kubwa la mafundi wababaishaji maarufu kama 'vishoka' ambao hawana leseni kutoka Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Wimbi hilo la vishoka, limesababisha EWURA kuanzisha mapambano dhidi yao, ambao wanafanya kazi za kuunganisha mifumo ya umeme bila leseni kwa kuwa uunganishaji usiozingatia utaalam husababisha madhara mbalimbali ikiwamo nyumba kuungua au kupata hitilafu za umeme kila mara.

Sheria ya Umeme nchini zinatekelezwa na Shirika la Umeme nchini(Tanesco) na EWURA, zinaweka wazi kwamba ni makosa mtu kuunganisha mifumo ya umeme bila ya kuwa na leseni kutoka EWURA.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, anasema sheria hiyo inamtaka mtu yeyote anayefanya kazi ya umeme bila leseni, adhabu yake ni kifungo cha miaka mitano au faini isiyozidi Sh. milioni 10, au adhabu zote mbili kwa pamoja.

"Sisi EWURA tunaendelea na mapambano dhidi ya mafundi wanaofanya kazi za kuunganisha mifumo ya umeme bila kuwa na leseni. Utoaji wa leseni za uunganishaji unalenga kuweka utaratibu wa kisheria," anasema.

Anabainisha kuwa hatua ya kutambua mafundi umeme wenye vigezo vya kupewa leseni, itasaidia serikali kutimiza azma ya kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na umeme kwa usalama zaidi kwa kuhudumiwa na mafundi wenye vigezo.

Mhandisi Chibulunje anasema wanalenga kukabiliana na wimbi la vishoka wanaounganishia watu umeme kinyume cha sheria, hivyo kusababisha madhara makubwa kwa usalama wa watu na mali zao.

"Maombi ya leseni ya umeme hufanywa mtandaoni kupitia mfumo uitwao 'Licensing and Order Information System (LOIS)' naopatikana kupitia tovuti ya EWURA," anasema.

Katika mfumo huo, anasema mwombaji anapaswa kuwa na nakala ya picha ya rangi ya bluu, wasifu, vyeti vya elimu ya ufungaji umeme, risiti ya malipo ya maombi ya leseni, hati ya kusafirisha au kitambulisho cha taifa na nakala za vyeti zilizothibitishwa.

"Baada ya kupokea maombi, EWURA huwasiliana na chuo alichosoma mwombaji ili kuthibitisha uhalali wa vyeti alivyowasilisha. Baada ya kupata uthibitisho, maombi ya leseni huwasilishwa katika kamati ya leseni za umeme ili kupata mapendekezo daraja stahiki la mwombaji wa leseni,"anasema.

Anabainisha leseni za umeme zinatolewa katika madaraja mbalimbali kulingana na sifa za mwombaji.

"Daraja A ni fundi mwenye uwezo wa kufanya shughuli zote za ufungaji na usambazaji umeme, daraja B ni ufungaji umeme msongo wa kati hadi volti 33,000, daraja C ufungaji umeme wa msongo usiozidi volti 400," anasema.

"Mengine ni daraja D ufungaji umeme wa msongo usiozidi volti 220, daraja W atafanya kazi chini ya usimamizi wa mwenye leseni daraja A,B,C au D, S1 ni daraja la kazi maalum za umeme kwa misongo yote."

Anafafanua S2 ni kazi maalum za umeme wa msongo hadi volti 33,000, S3 kazi maalum za umeme wa msongo hadi volti 1000.

Anasema EWURA imejipanga kuhakikisha wananchi wananufaika katika njia sahihi, kwa kuwa na wenye vigezo pekee katika kazi ya uunganishaji umeme wa nyumbani (kwenye makazi) pasipo kusababisha madhara ya kiuchumi, kijamii na kiafya.

Anataja miongoni mwa majukumu ya EWURA, ni kutoa leseni na kusimamia utekelezaji wake, kudhibiti ubora, usalama na tija kwa watoa huduma, kutathmini na kupitisha marekebisho ya huduma na kusikiliza malalamiko, pia kutatua migogoro.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, anasema mamlaka hiyo imekuwa ikifanya kazi kwa kuzingatia nyenzo za udhibiti ikiwamo sheria za sekta husika, ikiwamo Sheria za Umeme ya mwaka 2008, Mafuta ya 201) na ya Maji ya mwaka 2019.

Anakumbusha chimbuko la EWURA, ni uwepo wa mamlaka za udhibiti nchini unaotokana na mageuzi ya kiuchumi na sera ya ushindani na udhibiti ya mwaka 1999, inayotambua sekta binafsi katika utoaji mchango kwenye uchumi na kwamba taasisi za umma lazima zijiendeshe kibiashara.

Anasema ni lazima jamii ifahamu kuwa EWURA inadhibiti huduma za nishati (umeme, petroli na gesi asilia), maji na usafi wa mazingira, udhibiti anaojisifu umesaidia kupunguza gharama za udhibiti na kuwezesha mapato ya tozo ya sekta ya nishati, kugharamia sehemu ya gharama za udhibiti za sekta za maji.

Anabainisha EWURA imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi, kuhusu huduma hizo, lengo ni kuharakisha uelewa wa matumizi ya nishati za umeme na gesi majumbani.

Kaguo pia anasema uamuzi wa kutoa elimu kwa wadau ni kuwawezesha kufanya shughuli kisheria na kanuni zilizopo.

"Kuna wakati makandarasi huona kama wanaonewa kwa kuhitaji kusajiliwa na kupewa leseni, lakini ikumbukwe kuwa hili linafanyika nchi nzima kwa sababu za usalama na ndiyo maana kila mdau hana budi kutambuliwa na kupewa leseni," anasema Kaguo.

Kaguo anasema, umefika wakati Watanzania kuwa na utamaduni wa kuwatumia watalaamu wenye leseni za Ewura, kutandaza nyaya za umeme katika majengo yao, kuepuka hatari na hasara kwao na serikali.

### RIPOTI YA MWAKA 2018/19

Ripoti ya utendaji kazi ya sekta ndogo ya umeme iliyotolewa na EWURA mwaka 2018/19, inaonyesha mamlaka hiyo ilitoa leseni 662 kati ya hizo, 654 zilikuwa za ufungaji vifaa vya umeme na nane zilikuwa leseni za uzalishaji umeme.

Aidha, mamlaka hiyo ilitoa leseni za usakinishaji(installations) wa umeme 654 na 600 katika mwaka wa fedha 2018/19 na 2017/18, ambazo zinaongezeka kwa asilimia 8.2.

Pia Leseni 15 zilitolewa kwa wanawake na 639 kwa wanaume katika mwaka wa fedha 2018/19, wakati leseni 10 zilitolewa kwa wanawake na 590 kwa wanaume katika mwaka wa fedha 2017/18.

### KAULI ZA WANANCHI

Mmoja wa wakazi wa Dodoma, Robert Cheti, anasema anaunga mkono jitihada za mamlaka hiyo kudhibiti vishoka kwa kuwa wengi wanaofanya kazi bila leseni matokeo ya kazi zao yamekuwa chini ya kiwango, hali inayochangia ya madhara ndani ya muda mfupi baada majengo kukamilika.

Anasema mafundi wengi wasio na uwezo na elimu sahihi kuhusu vifaa umeme vinavyofaa, hujikuta wanaingia kwenye mtego wa kununua vifaa visivyokidhi viwango na kuishia katika majengo yaliyotajwa kwa jamii.

"Ni wakati muafaka kwa jamii kuhakikisha inashirikiana na mamlaka ya udhibiti kuhakikisha wimbi la vishoka katika jamii linaisha,"anasema.

HABARI KIMATAIFA

# WFP yashinda tuzo ya Nobel

**OSLOW, Norway**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Chakula Duniani (WFP), limepata tuzo ya amani ya Nobel ya mwaka huu.

Kamati ya tuzo hiyo inayotolewa nchini Norway, ilitaja WFP kuwa baada ya kuhusika katika juhudi za kuzuia njaa kugeuza kama silaha katika migogoro na vita. Mshindi anapata dola milioni 101 kama zawadi ya kutambua mchango wake.

Msemaji wa WFP, alisema shirika hilo linajivunia tuzo hiyo.

Shirika hilo linakadiria kusaidia watu milioni 97 kila mwaka katika mataifa 88.

"Kutokana na tuzo ya mwaka huu, kamati hii inataka dunia kuangazia mamilioni ya watu ambao wanakabiliwa na tishio la baa la njaa", alisema Mwenyekiti wa kamati ya tuzo hiyo, Berit Reiss Andersen.

BBC



Wanaharakati kutoka Chama cha Bhartiya Janata (BJP), wakijaribu kuvunja kizuizi cha polisi ambao walitumia maji yanayowasha kuwazuia kuingia ofisi ya Waziri Mkuu wa jimbo la Bengal Magharibi, Mamata Banerjee, kupinga sheria mpya. **(PICHA: AFP)**

# Armenia, Azerbaijan kujadili umalizaji vita

**MOSCOW, Urusi**

NCHI za Armenia na Azerbaijan, zimekubaliana kushiriki mazungumzo yao ya kwanza ya kumaliza mapigano katika jimbo la Nagorno-Karabakh.

Makubaliano yamefikiwa wakati wanajeshi wa pande mbili wanaendelea kushambuliana vikali ili kudhibiti mkoa huo unaogombaniwa.

Wizara ya mambo ya kigeni ya Urusi, ilisema wanadiplomasia waandamizi kutoka nchi hizo mbili, watashiriki mazungumzo hayo yatakayofanyika nchini humo katika mji mkuu wa Moscow.

Ilisema Rais Vladmir Putin, aliomba viongozi wa pande hizo kushiriki katika mkutano huo.

Hata hivyo, maofisa wa ulinzi wa Armenia na Azerbaijan walisema mapigano yaliendelea usiku wa juzi na kusababisha vifo vya raia.

Mpaka sasa zaidi ya watu 400, wameuawa tangu makabiliano ya silaha yalipozuka kati ya wanaharakati wa Armenia wanaotaka kujitenga na wanajeshi wa Azerbaijan mwishoni mwa mwezi uliopita.

DW.

# Hariri ahimiza kuufufua mpango wa uchumi

**BEIRUT, Lebanon**

WAZIRI mkuu wa zamani wa Lebanon, Saad al-Hariri, ametoa wito wa kurejeshwa kwa mpango wa kufufua uchumi uliotolewa na Ufaransa ili kuliondoa taifa hilo katika mgogoro.

Katika mahojiano ya televisheni, Hariri ambaye ni mfuasi wa dhehebu la Suni, alivitaka vyama vya kisiasa kutafakari vyema ili wasiipoteze fursa hiyo.

Alisema mpango wa Rais wa Ufaransa, Emmaniel Macron, bado upo na unaweza kutekelezwa.Ufaransa, ambayo ilikuwa koloni lake inaongoza juhudi za msaada wa kigeni kuokoa nchi hiyo, ilijaribu kuwahimiza viongozi wa Lebanon kufanya mageuzi ili kuukabili mzozo huo wa kifedha.

DW.

# Rais wa Kyrgyzstan akubali kujiuzulu

**BISHKEK, Kyrgystan**

RAIS wa Kyrgystan, Sooronbai Jeenbekov, amesema yuko tayari kujiuzulu baada ya baraza jipya la mawaziri kuteuliwa.

Nchi hiyo inakabiliwa na ombwe la madaraka na kuilazimu Urusi kutishia kuingilia kati kuhakikisha hali ya utulivu inadumishwa.

Kyrgyzstan, ambayo ina kituo cha jeshi la anga la Urusi, ilikumbwa na machafuko baada ya wafuasi wa upinzani walipoyakamata majengo ya serikali siku ya Jumanne ya wiki hii.

Upinzani ambao unawakilisha vikundi vya kikabila na koo mbalimbali, umepiga hatua ya kwanza kuelekea kuleta utulivu, na kuongeza matumaini ya kumalizika kwa mgogoro huo ambao umetishia uzalishaji wa madini ya dhahabu nchini humo.

Urusi ilieleza hali hiyo ya fujo na machafuko inajaribu kuharibu siasa za nchi zilizokuwa sehemu ya muungano wa kisovieti.

DW

# Raia Mali watakiwa kunusuru nchi yao

**NEWYORK, Marekani**

MJUMBE wa Umoja wa Mataifa kuhusu mgogoro wa Mali, Mahamat Saleh Annadif, amewaomba raia wa nchi hiyo kutumia muda wa mpito kuondokana na picha mbaya iliyosababishwa na mapinduzi ya kijeshi.

Nchi hiyo ya Afrika Magharibi, imeunda serikali ya mpito itakayodumu kwa muda wa miezi miezi 18, kabla ya kurudisha utawala wa kiraia.

Annadif, aliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kuwa mafanikio ya kipindi hicho cha mpito yanakaribia kupatikana, jukumu liko mikononi mwa watu wa Mali.

Mali imekuwa katika machafuko tangu vuguvugu la umma la mwaka 2012 lilosababisha wanajeshi waasi kumuondoa rais madarakani.

DW

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


Nipashe MWANGA WA JAMII

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GIDION ALIPIPI KASEGE** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **VOLVO** zenye namba za usajili **T 602 BTE** CHASSIS namba **YU/C291/G84105142 .** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. POLISI TAARIFA **DAR/CEN/RB/721093/2020**

115938902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA ILIYOPO DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 42 YA 2016**

**CATHERINE HONORATI............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **CRDB BANK PLC**
2. **METHOD KAUNGA MORIS**
3. **HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE................WAJIBU MAOMBI**

**KWA: HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE – POPOTE ALIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la rufaa ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama ya Rufaa hapa Dar es salaam tarehe 19/10/2020 saa tatu kamili asubuhi (3:00) katika ukumbi wa Mahakama ya Biashara. Unapaswa kuhudhuria siku ya tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hautahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi maombi yako yatasikilizwa bila ya uwepo wako.

**Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 1/10/2020**

E. G. Mrangu
Kny: **MSAJILI**
**MAHAKAMA YA RUFANI**

115938502

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**COSMAS ANDREA KIVUYO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA YA USAJILI **MC 963 CMH.** CHASSES NO **MD 621EP18 KIK 00972.** ENGINE NO **CPIKK1128619.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. **ARU/ARU/RB/726272/2020.**

115938702

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**HILDAGARDE JAMES CHEGE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE **INDEX No. S0297-0029** MWAKA 2011 SHULE- QUEEN OF FAMILY GIRLS SECONDARY SCHOOL. CHETI CHA KIDATO CHA SITA CHENYE **INDEX No. S0333-0628** MWAKA 2014 SHULE- MWANZA SECONDARY SCHOOL. CHETI CHA JESHI **AKD: 4640** MWAKA 2014 OLJORO **JKT(833KJ)** MAHALI VILIPOTEA NI DAR ES SALAAM. RB Number-**DOD/DOD/RB/316275/2019.**

115939002

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IDDA ANANIA SHOMARI** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 731 AVQ** aina yake **TOYOTA-HARRIER** yenye chassis namba **MCU100033727.** Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote Cha polisi. RB Namba **MOR/MOR/RB/700146/2020.**

115939702

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GIDION ALIPIPI KASEGE** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI SWIFT** zenye namba za usajili **T 258 AUZ** CHASSIS namba **HT515-612453.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. POLISI TAARIFA **DAR/CEN/RB/721087/2020**

115938902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA ILIYOPO DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 42 YA 2016**

**CATHERINE HONORATI...........................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **CRDB BANK PLC**
2. **METHOD KAUNGA MORIS**
3. **HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE................WAJIBU MAOMBI**

**KWA: METHOD KAUNGA MORIS – POPOTE ALIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la rufaa ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama ya Rufaa hapa Dar es salaam tarehe 19/10/2020 saa tatu kamili asubuhi (3:00) katika ukumbi wa Mahakama ya Biashara. Unapaswa kuhudhuria siku ya tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hautahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi maombi yako yatasikilizwa bila ya uwepo wako.

**Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 1/10/2020.**

E. G. Mrangu
Kny: **MSAJILI**
**MAHAKAMA YA RUFANI**

115938502

---

## Taarifa ya Kufungwa

**INATOLEWA TAARIFA KUWA** katika mkutano wa ziada wa **KARIMJEE CONSULTANTS LIMITED** uliofanyika siku ya **23rd day** of **December 2019**, azimio maalum lilipitishwa kwa pamoja na wamiliki/wanahisa wa kampuni la kufunga kampuni kwani haijafanya shughuli zake.

Ikiwa mtu ana madai yoyote au maslahi dhidi ya kampuni, wanashauriwa kuwasiliana na kampuni kwenye anwani iliyo chini ndani ya **siku 7** za taarifa hii.

Karimjee Attorneys
P.O. Box 76421
Dar es Salaam

115939202

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KIONDO MGWENO KAVUYU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina Suzuki Escudo yenye namba za usajili **T 471 DPY.** Chassis no. **TD54W104914.** Engine no. **J20A291608.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/726204/2020.**

115939602

---

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)
Katika Mahakama ya Mwanzo ya
**DODOMA MJINI**
Usimamizi wa Mirathi **No. 143/2020.**
Ombi la **AMAN JAMES MINJA**
kuteuliwa kuwa
Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu
**HELLEN FELIX MINJA**
KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe **02/11/2020** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe **09/10/2020.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**FRANK ISSACK SILAVWE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **T400 ARB XL.** Injini namba **1125s5737669** Taarifa yoyote itolewe kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **IRI/IRI/RB/725370/2020**

115938402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI.**

**Usimamizi wa mirathi No;256/2020**

**Ombi la MARIAMU ZAHORO ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ATHUMAN AHMAD MOHAMED.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 29/09/2020.

Tarehe 29/9/2020
Sahihi: HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115938802

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KAMUGISHA ANISETH BYABATO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **VOLKSWAGEN T4** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 957 BLZ.** CHASSIS NAMBA **VW2ZZZ702MHO22035.** YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/KIJ/RB/726604/2020.**

115938602

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO 53 OF 2020**

**In the matter of the Estate of the late ONESMO SALEHE MTEY of Dodoma municipality**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY KELVIN ONESMO MTEI**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 30th day of OCTOBER 2020
**Dated at Dodoma this day of 17th day of OCTOBER 2020.**

RESIDENT MAGISTRATE

115939402

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 51 YA MWAKA 2020**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**RASHMI MANJI BARMEDA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**NIMESHI RASHMI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**
Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya **tarehe 21** Mwezi wa **Octoba, 2020.**
Imewasilishwa Dar es salaam, leo **tarehe 21** Mwezi wa **Septemba, 2020.**

NAIBU MSAJILI

---


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini-**33**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

Saa ya ukutani ilionyesha kuwa ni saa saba mchana. Mlango uligongwa kwenye ofisi ya Eddy. aliingia mhudumu mmoja akiwa na bahasha nyeupe.

Alimsalimu bila kuongea kitu akamkabidhi. Aliiweka mezani kwa dakika moja kama mtu aliyeipuuzia.

Baada ya kumalizana na kompyuta, aliichukua barua na kuifungua. Aliisoma. Akaisoma tena. Akaisoma kwa mara nyingine tena.

Ilitoka kwa mamkala ya usajili ya magari nchini. Ilionyesha jina la mmiliki wa gari ambalo lilikwenda Kigogo kumtafuta Timo na kumpa kazi ya kumuua Fikiri.

Eddy alichotaka kujua ni mmiliki na si aliyeendesha. Alijua kumpata mmiliki kungemrahisishia kazi. Nani alimpa gari siku ile, au lilikuwa mikononi mwa nani kwa siku ile hadi linarejea kwa mmiliki.

Kwa mujibu wa namba ambazo kijana yule Timo alisema akizikariri kwa urahisi kutokana na kufanana na kiasi cha pesa alizolipwa, zilionyesha mmiliki wake ni George Kupila.

Halikuwa jina jipya. Aliwahi kulisikia mahali. "Ni Wapi?" Alijiuliza.

Alifungua droo na kutoa gazeti mwaka jana. Ilikuwa wakati wa mauaji ya Patiyo na mkewe Grace.

Gazeti liliandika aliuyeuawa bwana harusi aliitwa Patiyo Kupila na Grace Pius.

"Ina maana gari alilotumia dereva aliyekwenda kumtumia Timo kumuua Fikiri linamilikiwa na George Kupila. Fikiri ni yule aliyembamba na kifuko cha sumu. Sumu hiyo ndiyo iliyokutwa kwenye chakula ambacho Shani alitewa na Fikiri. Shani ni binti ya Patiyo Kupila. Je George na Patiyo ni ndugu? Alijiuliza.


"Nitamuuliza Shani, kwani hata yeye anaitwa Shani Patiyo Kupila." Aliinua simu na kumuuliza kama anamfahamu mtu anayeiwa George Kupila.

"Ndiyo Sherry, huyo ni baba yangu mdogo kabisa mama mmoja na baba mmoja." Kengele ya hatari ikaanza kugonga kwenye kichwa cha Eddy.

**************************************

Geti lilifunguliwa baada ya Eddy kupiga honi mbili. Tayari walinzi walishaambiwa kuwa kuna mgeni maalum anawasili.

Ilikuwa ni majira saa nne asubuhi. Siku hiyo Eddy alikwenda kazini alfajiri na mapema kuweka mambo sawa kwa sababu alijua mpenzi wake haendi kazini, hivyo baada ya kupunguza kazi aliamua kwenda Mbezi Beach kwa ajili ya kushinda naye, kula chakula cha




**Ina maana gari alilotumia dereva aliyekwenda kumtumia Timo kumuua Fikiri linamilikiwa na George Kupila. Fikiri ni yule aliyembamba na kifuko cha sumu. Sumu hiyo ndiyo iliyokutwa kwenye chakula ambacho Shani aliletewa na Fikiri. Shani ni binti ya Patiyo Kupila. Je George na Patiyo ni ndugu?**

mchana kama walivyoahidiana.

"Karibu Sherry." Shani alimkaribisha, akiwa amevaa nguo za uanamichezo.

"Kumbe huwa unafanya mazoezi?" Aliuliza Eddy.

"Mazoezi gani, basi tu tunapunguza shibe tu."

"Mhh, Sherry, mbona siku hizi naona kama unanenepa, tofauti na pale mwanzo?"

"Nanenepa eee." Shani alisema huku akijiangalia na kuonekana akifurahia jambo hilo, kisha akajibu.

"Siku hizi sina mawazo sana, kipindi kile nilikuwa na mawazo mengi, sina rafiki, na huwezi kulazimisha kuwa na rafiki na mtu ambaye humuamini..."

"Kwa hiyo mimi unaniamini sana eee."

"Yaani sijui umeniroga? Mimi nimetokea kukuamini sana wewe. Kama unanihujumu, au kumbe ndiyo adui yangu umekuja kunimaliza, sawa, sasa nitafanyaje, maana imeshakuwa hivyo." Shani alisema akimuangalia kwa makini Eddy.

Eddy aliangua kicheko. Akamtazama Shani akamwambia "Halafu nimekukuta umependeza sana leo."

Shani alimtazama mwenzake kwa kukunja sura "Mhhhh, muongo sema sijapendeza, unanionana nikiwa nimejipamba, leo hata nywele sijachana, niko hovyo hovyo, hata kuoga sijaoga, halafu unasema nimependeza."

"Mimi nakupenda wewe. Nakupenda vyovyote utakavyokuwa. Vyovyote utakavyovaa. Hajua wanawake mnapenda sana kujipamba na muda wote muonekane warembo, lakini mimi kwako nakupenda wewe tu basi, haijalishi umesuka nywele, haujasuka, umevaa vizuri, vibaya. Kwani ukivaa hata gunia, utakuwa siyo Shani?"

"Hata baba." Shani alishindwa kuendelea kubishana na Eddy. Wakati huo alikuwa amekaa kwenye sofa.

"Hebu njoo kwanza." Eddy alimwita kwa sauti iliyoonekana kama kuna kitu cha maana anataka kumwambia.

Shani alisogea kwa heshima zote. Eddy alimvuta. Akapapasa mikono yake laini, akabusu kwenye mashavu yake mororo.

Shani alitabasamu. Hakufikiri kama ndicho alichoitiwa na Eddy. "Ni hicho tu, haya fanya shughuli zako."

Aliondoka kwa kuringa, huku akigeuka nyuma kumtazama Eddy kwa jicho la huba. Ni kama vile alimwambia "Ngoja subiri nakuja."

"Naenda kuoga kwanza my, nisubiri, nikuwashie muziki, au nikupe kinywaji?"

"Ninakuhitaji wewe zaidi kuliko chochote kile ambacho utanipa." Eddy alimjibu.

"Haya subiri." Shani aliongea na kuingia kwenye vyumba vingine.

Ilipita kama dakika tano hivi. Eddy alihisi kitu ambacho si kawaida. Zilikuwa ni sauti za watu ambao wanaruka ukuta, japo walijitahidi kuruka bila vishindo.

Hakuna na uzoefu sana na nyumba hiyo, hivyo hakujua wamerukia upande gani na wanaelekea wapi.

Kutokana na uzoefu wa kazi yake, alihisi shari. Aliiangalia karanda hiyo kwa haraka, aliona kuna sehemu ambayo kuna friji ya maji, anaweza kujificha nyuma yake. Haraka akafanya hivyo.

Sekunde kadhaa baadaye, mlango mkubwa ambaye aliingilia yeye, ulikuwa na mtu mmoja mrefu mwembamba aliyekuwa ameufungua. Alikuwa ameshika bastola. Aliingia ndani na kujibanza pembeni macho yake yakiwa mbele kukabilia na chochote kitakachojitokeza mbele yake.

Nyuma yake aliingia mtu mwingine mfupi, mnene wa wastani. Hakuna na chochote zaidi ya kamba ya manila.

Kwa akili ya haraka na kwa uzoefu wake alijua kabisa walikuja kuua na si kuteka wala kutesa mtu.

Kwa jinsi sakata zima alilokuwa akilifuatilia kwa siri bila yoyote kujua, alijua kabisa kuwa Shani yupo kwenye matatizo.

Baada ya kuingia ndani, jamaa walibadilishana. Mwenye kamba alitangulia mbele, huku mwenye bastola akibaki nyuma. Walinong'onezana kitu, yule mfupi alisonga kule ambako Shani alikwenda.

Eddy akutaka chochote kibaya kimpate Shani. Hakutaka kuruhusu yule jamaa aingie afungue mlango na kutokomea ndani kwani hawezi kujua kule atakwenda kumfanya nini.

Damu ilimsisimka Eddy. Lakini pia alifurahi kuona siku hiyo angepata mazoezi ambayo kwa muda mrefu hajayafanya. Kucheza mchezo wa hatari ambao yeye anaupenda.

Kama umeme, alitoka sehemu aliyojificha. Wakati mwenye bastola alishtuka pembeni yake kuna nini, kwani alikuwa akiangalia zaidi mbele, alijikuta akipigwa teke mkononi ambalo lilirusha bastola juu, ikagonga juu na kuanguka chini. Ilikuwa kama sinema hivi. Eddy aliipiga tena teka bastola, ikaserereka na kuingia uvunguni mwa kochi. Ilionekana jamaa mrefu alikuwa yuko vizuri, kwani alirusha teke ambalo Eddy aliliona vizuri na kulipangua kwa mkono.

Kwa sababu jamaa hawakuwa tena na bastola, Eddy hakuwa na haraka, wakati akirusha ngumi aliikwepa.

Wakati huo, jamaa aliyekuwa anataka kuingia ndani aliahirisha na kurejea kumsaidia mwenzake.

Huyu ndiye Eddy alianza naye, kwani alijikuta akipigwa teke la mbavu lililomfanya aanguke chini kama gunia.

Mwingine alikuwa mbishi alizirusha mbili tatu, huku akiwa hajapigwa hata ngumi moja.

Eddy alitishia kama anapiga ngumi ya kushoto, akawepa kwenda kulia, huko ndiko alikokutana na ngumi na mkono wa kulia iliyomrusha na kichwa chake kujipigiza ukutani.

Taratibu alishuka chini na kuegemea ukutani huku akiwa amekaa.

Eddy alimfuata na kumtazama, akagundua kuwa hakuwa na maisha. Hakuhangaika naye. Alimgeukia mwingine aliyekuwa anagaagaa. "Wewe ni nani na umefuata nini?" Aliuliza.

Hakujibiwa. "Nyinyi ni akinanani na nani amewatuma kuja hapa?" Aliuliza lakini safari hii kwa hasira.

Mlango ulifunguliwa, Shani alitoka. Alichokiona kilimfanya apige kelele za woga kwa sauti kubwa na kurejea alikotoka, akisahau kabisa kufunga mlango.

Eddy hakuhangaika naye, alichofanya ni kuchukua kamba aliyokuja naye jamaa yule na kumfunga mikononi na miguuni. Aliporidhika alimgonga sehemu ambayo alijua atazirai wa muda wa robo saa hivi kabla ya kuzinduka.

Alienda chumbani kwa Shani na kumkuta amejikunyata kitandani akilia.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# USHINDI WA ARGENTINA WAMFURAHISHA LIONEL MESSI




**BUENOS AIRES,** Argentina

LIONEL Messi ameonyesha umuhimu wa ushindi na sio kiwango baada ya Argentina kuanza michuano ya kufuzu kwa Kombe la Dunia kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ecuador.

Messi kwa mara nyingine alikuwa shujaa wa Argentina pale jijini Buenos Aires Alhamisi, baada ya kufunga penalti dakika ya 13 katika mechi yake ya kwanza kwa nchi yake tangu Novemba mwaka jana.

Argentina ilipangiwa kuanza michuano ya kufuzu Kombe la Dunia kwa nchi za Amerika Kusini kuelekea Qatar 2022 Machi, mwaka huu, lakini mlipuko wa virusi vya corona ukasitisha mipango hiyo.

Miamba hao wa Amerika Kusini hatimaye wakarudi kwenye mashindano kwa mara ya kwanza na wakaendeleza rekodi ya kutofungwa mechi nane, tangu baada ya fainali ya michuano ya Copa America iliyomalizika Julai, mwaka jana. shukrani kwa bao la mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, Messi.

"Tulijua kwamba mambo yangekuwa magumu. Lakini jambo la muhimu ni kwamba tulishinda na tunatakiwa kufanya kazi kwa bidii na kuendelea kukua," alisema Messi mara baada ya mchezo huo.

"Ilikuwa muhimu kwa mwanzo mzuri kwa sababu tulijua kwamba kufuzu Kombe la Dunia ni kazi ngumu.

"Mechi zote zinakuwa ngumu. Tulitumaini tungeweza kucheza kwa utofauti, lakini ni zaidi ya mwaka sasa tangu tumecheza pamoja, huu ulikuwa ni mchezo wa kwanza kwa pamoja."

# Aouar afunguka anavyoipenda Lyon

**LYON,** Ufaransa

KIUNGO wa Lyon, Houssem Aouar, anasisitiza hajaumizwa na kitendo cha kukwama kwa mchakato wake wa kujiunga na Arsenal katika kipindi cha majira ya joto mwaka huu.

The Gunners iliwasilisha ofa mbalimbali kwa klabu hiyo ya Ufaransa lakini zilikataliwa baada ya thamani ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 22, kutangazwa ni pauni milioni 55.5.

Hata hivyo, Arsenal imefanikiwa kunasa saini ya Thomas Partey kwa dau la pauni milioni 45, katika siku ya mwisho ya dirisha la usajili.

Aouar, ambaye alikuwa kwenye kikosi cha Ufaransa kilichopata ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Ukraine katika mchezo wa Jumatano iliyopita, alisema ana furaha kubakia Lyon.

"Nimekuwa nikijiuliza mwenyewe maswali mbalimbali," alisema kiungo huyo.

"Nina nafasi ya kuwa na msimu wenye mafanikio ndani ya klabu hii na nafurahi kuona sijapoteza nafasi hiyo.

" Kuhuzunishwa? Niko katika upande wa pili. Mimi niko hapa nyumbani, katika klabu ambayo ninaipenda, pamoja na marafiki na familia yangu.

Aouar anaendelea kuwa mchezaji aliyekuwa anawindwa na Mikel Arteta na klabu hiyo inatarajiwa kuwasilisha ofa mpya ya kumsajili katika kipindi cha majira ya joto mwakani.







# Traore hafikirii kurudi Barca

**BARCELONA,** Hispania

WINGA wa Wolves, Adama Traore, amesisitiza hafikirii kurudi kuichezea klabu yake ya zamani ya Barcelona licha ya kufanya mazungumzo ya mara kwa mara na kinda wa klabu hiyo ya Camp Nou, Ansu Fati.

Traore alichipukia kwenye akademi ya Barca, lakini alishindwa kupata nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kwanza, lakini sasa anatamba pale kwenye dimba la Molineux baada ya kucheza kule Aston Villa na Middlesbrough.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ameendelea kuonyesha kiwango cha kuvutia akiichezea kwa mara ya kwanza Hispania Jumatano dhidi ya Ureno na kocha wake, Luis Enrique akamsifia kwa kiwango kizuri kwenye mchezo huo wa kirafiki.

Amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Barcelona awali, lakini yeye mwenyewe hana mpango wa kurudi katika klabu yake hiyo kwani bado anataka kucheza kule Wolves.

"Sio uamuzi yangu kama nafaa kucheza Barcelona. Akili yangu ni kucheza vizuri," alisema Traore akiwaambia waandishi wa habari.

Alipoulizwa kuhusu urafiki wake na Fati, ambaye aliweka rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuifungia Hispania, Traore alibainisha mazungumzo yao.

"Tunazungumza kila kitu," alisema. "Lakini sio jambo la kurudi tena Barcelona, uwezekano huo kwa sasa siuoni tena, lakini ni klabu iliyonilea."

# Loew apunguza wachezaji Ujerumani

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joachim Loew, amewapunguza wachezaji watano kutoka katika kikosi chake ambacho kitakabiliana na Ukraine na Uswisi katika Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Loew anaweka mategemeo yake katika uzoefu wa wachezaji wa Bayern Munich na RB Leizig wanaorejea katika kikosi hicho.

Ujerumani imepoteza uongozi mara tatu katika mchezo wa Uturuki na kutoka sare ya mabao 3-3 siku ya Jumatano, ambapo Loew alichezesha kikosi cha 'kujaziajazia' kutokana na wachezaji wake wengi kupewa mapumziko.

Ilikuwa ni mchezo wa tatu mfululizo ambapo Wajerumani walianza kwa kuongoza na kumalizikia kwa sare.

Pia ilikuwa ni mchezo ambao uliangaliwa na idadi ya chini kabisa ya watu katika televisheni tangu Loew aanze akiifunza timu hiyo kwa miaka 14 iliyopita.

Benjamin Henrichs, Nico Schulz, Niklas Stark, Nadiem Amiri na Mahmoud Dahoud, ambao wote walicheza dhidi ya Uturuki, wameondolewa katika kikosi hicho kabla ya mchezo wa leo, Jumamosi dhidi ya Ukraine na mchezo wa nyumbani dhidi ya Uswisi siku tatu baadaye.

Loew atakuwa na wachezaji wa Bayern, Joshua kimmich, Serge Gnabry, Niklas Suele, Leon Goretzka na mlinda mlango, Manuel Neuer katika kikosi hicho cha wachezaji 23 baada ya kupumzishwa pamoja na Marcel Halstenberg na Lukas Klostermann wa RB Leipzig.

Mshambuliaji, Timo Werner, ambaye amepata nafuu kutokana na ugonjwa, pia atarejea kama ilivyo kwa mchezaji wa kati wa Real Madrid Toni Kroos.

"Itakuwa ni muhimu kushinda michezo ijayo," Loew alisema.

"Kutakuwa bila shaka na timu tafauti kabisa uwanjani, kuliko dhidi ya Uturuki. Kila mmoja ana hamasa na morali ya kushinda."





# GIROUD KUONDOKA CHELSEA JANUARI

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Olivier Giroud anatarajiwa kuondoka klabuni hapo wakati wa dirisha dogo la Usajili Januari.

Hiyo ni baada ya nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza cha Cheslea kuwa finyu zaidi pale Staford Bridg.

Giroud mweye umri wa miaka 34, amekuwa anawindwa na Inter Milan ambayo inafundishwa na Antonio Conte ambaye aliwahi kumfundisha akiwa Chelsea, hivyo anamhitaji akiamini anaweza kucheza kulingana na mifumo yake.

Mbali ya Inter, Juventus pia ipo kwenye harakati za kuwania saini ya nyota huyo na Chelsea ipo tayari kusikiliza ofa kutoka klabu yoyote kwa kuwa umri wa mchezaji huyo umeenda sana na kocha Frank Lampard anataka kutengeneza timu kupitia vijana.

Mkataba wa mchezaji huyo unatarajiwa kumalizika mwakani huku thamani yake katika soko la usajili ni euro milioni saba.

# Ozil aachwa kikosi cha Arsenal Europa

**LONDON,** England

ANGUKO la Mesut Ozil limeendelea baada ya kuachwa kwenye kikosi cha Arsenal kitakachoshiriki mashindano ya Ligi ya Europa.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2014 aliachwa kweye kikosi cha wachezaji 24 kilichowasilishwa kwenye Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA), ambapo washikabunduki hao watacheza dhidi ya Rapid Viena, Dundalk na Molde.

Ozil mwenye umri wa miaka 31, hajajumuishwa kwenye kikosi cha Arsenal katika mechi sita za Ligi Kuu England na Kombe la EFL msimu 2020-21, na hajatokea katika klabu hiyo tangu Machi mwaka huu, wakati mashindano yote yaliposimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Kulikuwa na pendekezo kwamba, Ozil angeweza kuondoka katika uhamisho wa dirisha la kipindi cha majira ya joto lililofungwa Jumatatu iliyopita, lakini mshahara wake wa pauni 350,000 kwa wiki unaonekana kuwa kikwazo.

Mkataba wake wa sasa na klabu hiyo utamalizika mwakani.

Kikosi kamili cha Arsenal cha Europa: Bernd Leno, Runar Runarsson, Matt Macey, James Hillson, Dejan Iliev; Hector Bellerin, Gabriel, Rob Holding, Cedric Soares, Shkodran Mustafi, Calum Chambers, Pablo Mari, David Luiz, Sead Kolasinac, Kieran Tierney; Dani Ceballos, Willian, Ainsley Maitland-Niles, Thomas Partey, Mohamed Elneny, Granit Xhaka; Alexandre Lacazette, Pierre-Emerick Aubameyang na Nicolas Pepe.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA: NDOTO YANGU NI KUICHEZEA MADRID

Pia kiungo huyo Mfaransa afunguka uamuzi wake wa kutosaini mkataba mpya na United...

**MANCHESTER,** England

KIUNGO, Paul Pogba amesema ana ndoto za kuichezea Real Madrid na hana mpango wa kuongeza mkataba wake na Manchester United.

**United ilimnunua Pogba kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 89 kumsajili tena kutoka Juventus mwaka 2016, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ameshindwa kung'ara tofauti na matarajio waliyoyaweka juu yake.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 alifurahia msimu mzuri wa 2018-19, akifunga mabao 13 na kutoa pasi za mwisho tisa katika mechi 35 za Ligi Kuu England, kwa msimu mmoja.

Hata hivyo, amekuwa akikabiliwa na majeruhi ya mara kwa mara, na amehusika katika mabao manne tu (moja akifunga na kutoa pasi za mwisho tatu) kwenye mechi 19 za Ligi Kuu England, tangu kuanza kwa msimu kwa 2019-20.

Pogba ameonyesha nia yake ya kutaka kupata changamoto mpya licha ya mpango wake wa kuondoka pale Old Trafford bado haujafanikiwa.

Kurudi Juventus na kwenda Madrid ndio kumekuwa kukipamba vyombo vya habari, na Pogba amebainisha ndoto zake za kutaka kucheza kwenye Ligi Kuu Hispania, maarufu LaLiga.

"Wachezaji wote wangependa kuichezea Real Madrid. Ni ndoto kwa upande wangu. Kwanini isitokee siku moja?" alisema Pogba wakati akiwa na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Alhamisi.

"(Lakini) mimi nipo Manchester na naipenda klabu yangu. Nacheza hapa Manchester, naamini mambo yatakuwa bora na siku moja nitaondoka.

"Kwa sasa, mimi ni Manchester na ninaelekeza nguvu zangu kwa klabu hii na nitahakikisha ninarejea katika ubora wangu. "Nafikiri kuna wakati klabu hiyo itakuja kufanya mazungumzo na mimi na naamini watakuja na ofa nzuri, au isiwe hivyo.

"Kwa wakati huu hakuna ambacho kimeshafanyika, siwezi kukueleza kitu ambacho sikijui."

Pogba yuko katika majukumu yake ya Timu ya Taifa ya Ufaransa na baadaye atarejea England kuendelea kuitumikia Manchester United na mchezo wao utakaofuata utakuwa ni dhidi ya Newcastle United.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL, OZIL KUTETA

ARSENAL inataka kuanza upya mazungumzo ya kuvunja mkataba na kiungo wake Mjerumani, Mesut Ozil (31), kabla ya dirisha la usajili la Januari halijafunguliwa. ***(Mail)***

### CITY KUMBANA BRUYNE

MABOSI wa Manchester City wanaanza kutayarisha mazungumzo na kiungo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Kevin de Bruyne. Klabu hiyo inataka kumpa nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, mkataba mpya wa miaka mitano. ***(Times - subscription required)***

### UPAMECANO AGOMBEWA

MANCHESTER United inatarajia kufanya mchakato wa kumsajili beki wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Dayot Upamecano (21), kwa dau la pauni milioni 36.5 katika majira ya joto mwakani. Liverpool na Manchester City pia zinamwania beki huyo. ***(Bild, via Sun)***

### DEPAY AIOTA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Lyon na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay (26), amesema "mlolongo wa kanuni" ulisababisha akashindwa kujiunga na Barcelona katika dirisha la usajili lililomalizika. ***(AS)***

### AOUAR MOYO BARIDI

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Houssem Aouar (22), amesema hajahuzunika baada ya mchakato wa kuondoka Lyon kwenda Arsenal kushindikana. ***(Mail)***

### SARRI ANUKIA FIORENTINA

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Juventus, Maurizio Sarri anatajwa kuwa mmoja wa makocha wanaoweza kutua katika kikosi cha Fiorentina. ***(Tuttomercato - in Italian)***

### BALE AFIKIRIA MAKUBWA

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale (31), amesema anataka kutwaa taji la Ligi Kuu England msimu huu, akiwa na Tottenham Hotspur, wakala wa mchezaji huyo amesema. ***(Sky Sports)***

### CUISANCE ATUA MARSEILLE

KIUNGO Mfaransa, Michael Cuisance (21), amekanusha taarifa za kufeli vipimo vya afya, ambavyo vilisababishwa ashindwe kujiunga na Leeds United. Hata hivyo nyota huyo amejiunga na Marseille kwa mkopo akitokea Bayern Munich. ***(Sky Sports)***

### WILSON NJIA MOJA

LIVERPOOL inatarajia kufanya mazungumzo na winga wake, Harry Wilson kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kupelekwa kwa mkopo katika klabu nyingine baada ya kurejea kuitumikia timu yake ya Taifa ya Wales. ***(Standard)***

### SHEFFIELD YAMTAKA BROOKS

MABOSI wa Bournemouth hawatakubali kuona kiungo wa Timu ya Taifa ya Wales, David Brooks anaondoka klabuni hapo kabla ya dirisha la usajili la ndani halijafungwa. Sheffield United inamhitaji winga huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

## Mikakati tenisi walemavu yaiva

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Tenisi kwa watu wenye ulemavu kimeahidi kutumia misaada ya viti waliyopokea kuimarisha mchezo huo katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Tanzania ilipokea viti 10 kutoka katika Shirikisho la Tenisi Duniani (ITF), kwa lengo la kusaidia maendeleo ya mchezo huo.

Akizungumza na gazeti hili jijini, Dar es Salaam jana, Kocha wa Timu ya Taifa ya Tenisi kwa watu wenye Ulemavu, Riziki Salum, alisema msaada huo wameupokea kwa wakati na wameshajipanga kutekeleza mipango hiyo.

Riziki alisema tayari wameshaanza mchakato wa kuandaa programu za mafunzo kwa lengo la kuwafikia walengwa kwa wakati.

"Hivi viti vitatusaidia kuanza katika mipango yetu ya kwenda mikoani, ukizingatia tenisi kwa wenye ulemavu mikoani ni nadra sana, kwa sababu ya kukosa elimu lakini pia kutokuwa na vifaa vya michezo ikiwamo viti," alisema Riziki.

Alitaja baadhi ya mikoa, ambayo wataanza kupeleka mafunzo ya mchezo huo ni pamoja na Arusha, Dodoma, Morogoro, Mwanza, Tabora, Kilimanjaro na Mtwara.

## Evarist, Vunjabei kupanda ulingoni

**Na Adam Nyangasa,** TUDARCo

BONDIA Mtanzania, Innocent Evarist, anatarajia kupanda ulingoni kupambana na Prince Patel kutoka England katika pambano la kuwania ubingwa wa dunia litakalofanyika Oktoba 16, mwaka huu hapa jijini, Dar es Salaam.



Bingwa wa pambano hilo atakabidhiwa mikanda miwili inayotambuliwa na WBO Afrika, pamoja na WBO Global.

Rais wa Shirikisho la Ngumi za Kulipwa Nchini, (PST ), Emmanuel Mlundwa, alisema maandalizi ya mapambano hayo yanaendelea vizuri na michezo hiyo itafanyika kwenye Viwanja vya Mabembeani Keko jijini.

Mlundwa alisema pia kutakuwa na mapambano mengine ya utangulizi, ambayo yatawakutanisha Julius Kisaree dhidi ya Msabaha Salum wakati mwanadada, Halima Vunjabei (pichani) atachuana na Sunan Kumar kutoka India.

Alitaja mapambano mengine yatakuwa ni kati ya John Brendan dhidi ya Issa Mbwana, ambao watachuana kuwania mkanda wa Taifa.

Alisema hakutakuwa na kiingilio katika kushuhudia mapambano hayo na lengo la kufanya hivyo ni kuwafanya wapenzi wa ngumi na watu wengine kujumuika pamoja kupata burudani ya mchezo huo, lakini pia kutoa fursa kwa wajasiriamali wadogo kufanya biashara zao.

# YANGA YAELEZA SABABU LAMINE KUWA NAHODHA

**Na Adam Fungamwangwo**

KLABU ya Yanga imesema imeteua manahodha wake kutokana na mapendekezo ya benchi la ufundi, huku vigezo vya kitaalamu na kiufundi vikichukua nafasi na si vinginevyo.

Juzi Yanga ilimtangaza beki wa kati, raia wa Ghana, Lamine Moro kuwa nahodha mkuu, beki Mtanzania, Bakari Mwamnyeto kuwa msaidizi wake na kiungo kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Mukoko Tonombe kuwa msaidizi namba mbili.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema ni kweli benchi la ufundi lilitoa mapendekezo kuhusiana na uteuzi huo na uongozi ukaridhia na kuutangaza rasmi.

"Unajua nahodha ni lazima awe na vigezo fulani, lakini pia nidhamu, tumeona hawa wamekidhi hivyo vilivyoangaliwa na benchi la ufundi kutokana na mapendekezo, na ndiyo maana tukawapitisha na kuwa tangaza," alisema Bumbuli.

Alisema kuwa haina maana waliokuwa manahodha kabla, ambao ni Deus Kaseke na Haruna Niyonzima hawana vigezo hivyo, ila waliwaongoza wenzao kwa muda kwenye kikosi hicho.

"Manahodha halisi walikuwa ni Papy Tshishimbi na Juma Abdul, sasa kwa sababu wote waliondoka, ndiyo wakapewa Kaseke na Haruna kwa muda wakati wanatafutwa wengine," Bumbuli alisema.

Kabla ya Tshishimbi ambaye anajiandaa kujiunga na AS Vita ya DRC, kitambaa cha unahodha kilikuwa kinavaliwa na Ibrahim Ajibu, ambaye amerejea kwenye klabu yake ya zamani Simba.

Ajibu pia aliuchukua unahodha wa klabu hiyo aliyopewa na aliyekuwa Kocha Mkuu wa zamani, Mwinyi Zahera kutoka kwa Kelvin Yondani ambaye naye kwa sasa hayupo kwenye kikosi hicho.

Mpaka sasa Lamine, nahodha mpya wa Yanga amefunga magoli mawili kwenye mechi tano za Ligi Kuu, ambazo timu yake imecheza.



Viungo wa Azam FC, Frank Domayo (kulia) na Mudathir Yahya, wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mwadui FC itakayochezwa Jumatano. **PICHA: MTANDAO**

# KVZ yazifuata Simba, Yanga Dar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KVZ imeelekea jijini, Dar es Salaam kwa ajili ya kuweka kambi ya muda wa wiki mbili ili kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar inayotarajiwa kufanyika kuanzia Novemba 7, mwaka huu, imeelezwa.

KVZ ambao ni mabingwa wa Kombe la FA Zanzibar, watafungua msimu mpya kwa kuwavaa wafalme Mlandege katika mechi ya Ngao ya Hisani itakayochezwa Novemba Mosi, mwaka huu kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa 'Maafande' hao wa KVZ, Khamis Abdul-hamid, alisema lengo la kambi hiyo ni kuwaimarisha wachezaji wao kuelekea msimu mpya na kuhakikisha wanaibuka na ushindi katika mechi hiyo ya ufunguzi.

Abdul-hamid alisema pia wanajiimarisha na kujiweka imara kuelekea mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika watakayoshiriki baadaye mwaka huu.

Alisema katika muda huo wa mazoezi, wanatarajia kucheza mechi sita za kirafiki na timu mbalimbali za Dar es Salaam, ambazo zitawasaidia kuwajenga wachezaji wao, haswa wale wapya ambao wamesajiliwa hivi karibuni katika kikosi hicho.

Alieleza wamepeleka barua za kuomba mechi za kirafiki dhidi ya Simba, Yanga, Azam pamoja na klabu nyingine, ambazo watakubali maombi yao kwa lengo la kukijenga imara kikosi chao.

"Tumeamua kucheza mechi nyingi za kirafiki na timu za Ligi Kuu Bara, ili kukipima kikosi chetu, timu zetu za Zanzibar tumelingana viwango, ninaamini kama tutazipata mechi hizi, basi tutakuwa na kikosi bora na kilichojiandaa kuelekea msimu mpya," alisema kiongozi huyo.

Kikosi cha KVZ chenye wachezaji 30 kimeweka kambi katika Chuo cha Polisi Kurasini.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 10, 2020

Nipashe




Pogba: Ndoto yangu ni kuichezea Madrid UKURASA 22



Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Jack Grealish (kulia), akijaribu kumtoka beki wa Wales, Roberts, katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa kwenye Uwanja wa Wembley jijini, London juzi usiku. England ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA, KAZE MAMBO SAFI

## ●●● Anatarajiwa kuwasili nchini mapema kuiwahi Prisons, kubadilisha mfumo...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi cha Yanga kikiendelea kucheza mechi za kirafiki ili kujiimarisha, kocha wake mpya, Cedric Kaze, raia wa Burundi anatarajiwa kuwasili nchini wiki ijayo, ili kuanza kukinoa kikosi hicho.

**Kaze anatua Yanga kuchukua mikoba iliyoachwa na Zlatko Krmpotic, ambaye alitimuliwa nchini baada ya uongozi wa Yanga kutoridhishwa na kiwango cha timu yake.**

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana zilisema mazungumzo kati ya Yanga na Kaze, yako kwenye hatua za mwisho na uwezekano wa kutua nchini ni mkubwa. Chanzo hicho kilisema kuwa tayari kocha huyo ameshawajulisha marafiki zake, ambao baadhi yao ni makocha, uamuzi wake wa kujiunga na Yanga, ambayo ina kiu ya kusaka ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao.

"Kaze atakuja nchini wiki ijayo," kilisema kwa kifupi chanzo chetu.

Hata hivyo, Kaze alishindwa kuliambia Nipashe chochote kuhusiana na mchakato wa kujiunga na Yanga.

"Subiri, nitakwambia mambo yakiwa tayari, ila tumeshafanya mazungumzo nao," alisema kocha huyo.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, aliliambia gazeti hili, Kaze atatua nchini wakati wowote kuanzia sasa, ili kuanza majukumu yake mpya mara moja.

**SOKA BURUDANI**

Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Burundi (FFB), Ramadhan Kibuga, alisema jana kuwa Kaze ni kocha, ambaye anapenda mfumo wa pasi fupi na endapo Yanga itakubali kumpa muda atawatengenezea kikosi cha ushindani.

Kibuga alisema anaamini kocha huyo atatua kuanza kuifundisha Yanga lakini akamsifia ni mmoja wa walimu wachache kutoka Burundi, ambao wanaaminika kuwa na uwezo mzuri katika kazi yao.

"Tunajivua kutoka makocha mbalimbali, yupo Ndayiragije (Etienne) anaifundisha Taifa Stars, Hitimana Thiery yeye yuko na Namungo, timu yetu ya Taifa yuko Mrundi (Ndayizeye Jimmy), ni jambo la kujivunia," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza uwezo wa makocha wao wa ndani, umesaidia kupeleka wachezaji wengi Ulaya na anaamini, uwapo wao utasaidia pia kuinua soka la Tanzania.

Baada ya Taifa Stars kumaliza majukumu yake, Yanga itashuka dimbani Oktoba 22, mwaka huu kuwakaribisha Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga yenye pointi 13, iko kwenye nafasi ya tatu ikiwa nyuma ya Simba wanayolingana pointi huku vinara ni Azam FC yenye pointi 15.

## Stars, Burundi tambo kibao

**Na Saada Akida**

USHINDI ndio jambo pekee, ambalo kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kinawaza kuelekea mchezo wa kirafiki wa kimataifa, dhidi ya Burundi utakaofanyika kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Kocha Msaidizi wa Taifa Stars, Selemani Matola, alisema wamejipanga vizuri kusaka ushindi, ili kuwapa raha Watanzania katika mchezo huo, ambao wanajua utakuwa na ushindani.

Kiungo huyo wa zamani wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Matola alisema wameandaa kikosi cha mapambano na lengo la kila mmoja ni kutafuta matokeo mazuri. Alisema wachezaji wote wako fiti, isipokuwa mshambuliaji, John Bocco ambaye ni majeruhi pamoja na Himid Mao aliyetarajiwa kuwasili nchini jana, ili kuungana na wenzake kwa ajili ya mechi hiyo.

"Mechi itakuwa yenye ushindani mkubwa kwa sababu timu zote mbili zimejiandaa vizuri, ili kupata matokeo chanya, hatuogopi kwa kuwa na wachezaji wengi wanaocheza nje, kwani hata sisi tunao wachezaji wanaocheza nje ya Tanzania, hatutawahofia nyota wao," alisema Matola.

Naye Nahodha Msaidizi wa Taifa Stars, Aishi Manula alisema wachezaji wote wamejiandaa vizuri kupambana na Burundi na wako tayari kuhakikisha wanawapa mashabiki wao matokeo ya furaha.

"Tumejipanga kuonyesha kile tulichopewa katika mazoezi, hatuhofii wenzetu kuwa na wachezaji wengi wanaocheza nje sababu tunajiangalia sisi tunafanya nini na sio wao," alisema Manula.

Kocha Mkuu wa Burundi, Jimmy Ndayizeye, alisema wamejiandaa vizuri na wanahitaji ushindi katika mechi hiyo ambayo kwao wanahitaji kulipa kisasi.

Ndayizeye alisema ana imani utakuwa mchezo mzuri na wa kujipima nguvu sababu anafahamu Tanzania na Burundi ni marafiki halafu viwango vya soka vinalingana.

"Tumepata mechi tatu kwa nchi tofauti, ila tumechagua Tanzania sababu tunapata kipimo tosha na kusaidia timu yetu kufanya vizuri huko mbele," alisema Ndayizeye.

Nahodha wa Burundi, Berahino Saido alisema wamejipanga kuonyesha soka la ushindani, ili kuwasaidia kupata ushindi katika mechi hiyo ya kesho.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >